# Nipashe

Ijumaa Desemba 15 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581525

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**WAZIRI** aamua ma-DED wafutiwe barua za onyo



UKURASA 4

**TANZANIA** kujenga meli safari kwenda Comoro, Shelisheli

UKURASA 8

**ISRAEL:** Hatusikii hata tukitengwa tutaitwanga Gaza

UKURASA 19



BUFE

Nipashe

IJUMAA DESEMBA 15, 2023

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Tusipoangalia Historia ya Uhuru itapotea

ISEMAJI SERIKALI VS TAMWA WALIPOKAA MEZA MOJA ...

Darasa la R4, falsafa anayoitumia Samia kuisuka nchi kimaendeleo



UKURASA 11

# HATIMAYE

**KORTI** Kuu yatoa hukumu ya kina Mdee.....*Endelea ukurasa 2*



## UVIKO-19 katika kasi mpya, malaria Z'bar yarejea, yaua





UKURASA 3

UKURASA WA 24

## MBANGOSSOUM KATIKA HESABU ZA BENCHIKHA

WAKATI Simba inatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, klabu hiyo inatajwa...

## USA yarejesha msaada baada ya miaka saba

UKURASA 3

**MICHEZO** **WACHEZAJI YANGA WAITISHA MTIBWA** UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Hatimaye hukumu kesi ya kina Mdee yatolewa

**Na Grace Gurisha**



MAHAKAMA Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam imetengua uamuzi wa Baraza Kuu la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuridhia uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho kuwavua ubunge Halima Mdee (pichani) na wenzake 18.

Baraza hilo lililosikiliza rufani ya wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia chama hicho, lilibariki wabunge hao kuvuliwa uanachama wa CHADEMA uliofanywa na Kamati Kuu ya chama hicho.

Hata hivyo, Mahakama Kuu imesisitiza kuwa haijafuta uamuzi wa Kamati Kuu ya kuwavua uanachama wa CHADEMA Mdee na wenzake 18 kwa sababu walipewa nafasi ya kujieleza kwenye kamati hiyo, lakini hawakutumia.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Jaji Cyprian Mkeha wa mahakama hiyo, aliyeanza kwa kutoa ufafanuzi kwamba anajua watu wengi, wakiwamo mawakili, walikuwa wanafuatilia shauri hilo ili kujua kama ubunge wa wabunge hao ni halali au si halali.

"Jamani, shauri lililokuwa mbele yangu ni kwamba waleta maombi, yaani Halima Mdee na wenzake walileta maombi ya kuomba nafuu.

"Waliomba mambo mawili kwamba mahakama ifute uamuzi wa Kamati Kuu na uamuzi wa Baraza Kuu la CHADEMA. Kwahiyo, hilo shauri lingine hapa kwangu halipo," alisema Jaji Mkeha.

Alisema mambo mengi yaliwasilishwa na pande zote wakati shauri hilo linasikilizwa. Hoja hizo zilizalisha mambo matano ambayo yeye aliyapatia majibu.

Alisema kuwa katika jambo la kwanza, alijiuliza 'Je, mjibu maombi wa kwanza (CHADEMA) kanuni zake zilikuwa zinaruhusu kusikiliza kwa dharura? Kwa sababu waleta maombi (Mdee na wenzake 18) walisema hawakupewa nafasi ya kusikilizwa.

"Na kama kanuni zinaruhusu, Je, waleta maombi walipewa nafasi ya kusikilizwa? Na je, Kamati Kuu ilikuwa na hayo mamlaka ya kusikiliza mashauri kwa dharura?.

"Majibu yangu hapa ni ndiyo kwamba kanuni zinaruhusu usikilizwaji wa dharura na pia waleta maombi walipewa nafasi ya kujieleza, lakini hawakutumia nafasi hiyo," alisema Jaji Mkeha.

Vilevile, alisema, 'ukipewa wito, ukaomba ahirisho, si lazima jibu liwe moja tu la upande wako, kwa sababu kuna kukubaliwa na kukataliwa. Mdee na wenzake waliomba ahirisho, lakini lilikataliwa na kamati.

"Ikiwa kila mtu akipewa nafasi ya kusikilizwa, halafu hakutokea, akaomba ahirisho limekataliwa. Mwisho wa siku uamuzi utoke kwa upande wake, unaweza 'ukaparalaizi' (ukapooza) mashauri yote yaliyokuwapo mahakamani," alisema.

Alisema, "hoja nyingine ni je, waleta maombi walisikilizwa na Baraza Kuu? Jibu langu ni ndiyo, kwa sababu waliwasilisha rufani zao kupinga uamuzi wa Kamati Kuu kuwavua uanachama, lakini shida ambayo ilikuwapo wanalalamika kwamba kuna baadhi ya wajumbe walikuwapo kwenye vikao vyote viwili.

"Hili halikubaliki sehemu yoyote ile; yaani watu waliokuwapo kwenye Kamati Kuu, wakae tena kwenye Baraza Kuu kutoa uamuzi. Hii haiko sawa kabisa, lakini kwa Sheria za Bunge ndiyo zinaweza kuruhusu hili. Kwahiyo, ninakataa uamuzi wa Baraza Kuu ambao ulisikiliza rufani hiyo."

Mdee na wenzake 18, katika suala hilo hilo walikuwa wanalalamika kwamba Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika walishiriki kikao cha Kamati Kuu kisha kushiriki kikao cha Baraza Kuu la chama kilichobariki wao kuvuliwa uanachama.

Kutokana na hoja hiyo, Jaji Mkeha alifafanua kwamba kilichoamuliwa na Mahakama Kuu si kufuta uamuzi wa Kamati Kuu, bali kanuni za kisheria za haki ya kusikilizwa hazikupewa nafasi, hata kutengua sehemu ya mchakato unaotakiwa.

Alisema Mdee na wenzake walipewa nafasi ya kusikilizwa, lakini hawakutokea. Hata viapo vyao, wote walikiri kupokea taarifa ya Katibu Mkuu, Mnyika, iliyowataka wafike kwenye kikao hicho.

Nimetoa amri kwa Chadema kuzingatia utaratibu wa kanuni asilia za haki. Kila upande utabeba gharama zake na rufaa iko wazi kwa upande ambao haujaridhika na uamuzi huu," alisema Jaji Mkeha.

Alisema Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, matokeo yake rasmi yanatangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kufuata Ibara za 67, 68 na 78 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia Kifungu 89 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

"Likishapita hili, basi vyama vyote, ikiwamo CHADEMA, vinaanza mchakato wa kupeleka mapendekezo NEC kwa ajili ya viti maalum, ambapo na yenyewe itatangazwa kwa kufuata mtiririko uleule na kisha wanapeleka bungeni na Spika anasoma.

"Novemba 24, 2020, hawa waleta maombi 19, kupitia runinga ya TBC walionekana wakila viapo. Uongozi wa CHADEMA ulistaajabu kwa sababu haukuwa umefanya mchakato huo na Mwenyekiti akatoa taarifa kwa waandishi wa habari kwamba hawatambui wabunge hao," alisema.

**ILIVYOKUWA KORTINI**

Kulikuwa na taarifa kwamba uamuzi wa mahakama hiyo ungelitolewa jana saa nne asubuhi, lakini baadaye taarifa ilitolewa ikibainisha kuwa mahakama ilipanga kutoa uamuzi saa 8:30 mchana.

Hali hiyo ilisababisha baadhi ya wanachama na wafuasi wa CHADEMA waliokuwa wamefurika katika viunga vya mahakama, kutawanyika na wengine kubaki mahakamani kusubiria uamuzi.

Saa sita mchana, baadhi ya wanachama walianza kukusanyika katika eneo la mahakama wakiwa na shauku kujua kama Mdee na wenzake 18 ni wabunge halali au la.

Saa 8:39 mchana, waandishi wa habari na wanachama wa CHADEMA waliojitokeza kwa wingi na mawakili 13 waliingia kwenye chumba cha wazi namba nne (4) ambako kilikuwa kidogo kutokana na watu kuwa wengi. Joto lilikuwa kali, lakini hakuna aliyejali.

Jaji Mkeha aliingia mahakamani saa saa 8:42 mchana. Alianza kwa kuomba radhi kwamba chumba cha mahakama ni kidogo na hiyo imetokana na kwamba mahakama za wazi ambazo ni kubwa, zilikuwa na kesi za tuhuma za ugaidi zinaendelea. Aliomba watu wawe wavumilivu.

"Msije mkaona tumewanyima ukumbi mkubwa wa wazi, hapana! Hii inatokana na kesi za tuhuma za ugaidi zinaendelea katika vyumba vikubwa vya wazi vya mahakama. Msije mkaona tumefanya makusudi. Kwahiyo, mliokosa nafasi, itabidi msimame.

"Sasa ninaanza kusoma uamuzi kama nilivyouandaa kwa lugha ya Kiingereza, lakini nikishamaliza mwishoni, nitatoa ufafanuzi kwa Kiswahili ili kila mmoja aelewe kama haukuelewa vizuri lugha ya Kiingereza," alisema.

Kutokana na kauli hiyo, mwandishi aliona tabasamu kwa watu wengi. Jaji Mkeha alianza kusoma uamuzi huo kwa Kiingereza kuanzia saa 8:50 mchana hadi saa 11:06 jioni, huku akiwa anajifuta jasho na kunywa maji kutokana na hali ya hewa iliyokuwamo katika chumba hicho.

Kwa muda wote huo kulikuwa na utulivu mkubwa katika chumba hicho. Kuanzia saa 11:07 jioni, Jaji Mkeha alianza kuchanganua uamuzi wake kwa lugha ya Kiswahili hadi saa 11:50 jioni.

Baada ya kumaliza, jaji huyo aliwashukuru mawakili kwa ushirikiano wao waliompa tangu kesi hiyo ilipoanza. Alipotoka tu, baadhi ya wanachama walionekana kufurahia na kudai kuwa bado Mdee na wenzake 18 si wanachama wa CHADEMA.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi hiyo Julai 21, 2021 dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), wakiomba pamoja na mambo mengine, mahakama ipitie mchakato na uamuzi dhidi yao kisha itoe amri tatu.

Kamati Kuu ya CHADEMA iliwavua uanachama wa chama hicho Novemba 27, 2020. Walikata rufani Baraza Kuu kupinga uamuzi huo wa Kamati Kuu, lakini Baraza Kuu katika uamuzi wake wa Mei 11, 2022, lilitupilia mbali rufani yao hiyo.

Baada ya uamuzi huo wa Baraza Kuu, ndipo wakakimbilia mahakamani ambako kwanza waliomba na wakapata kibali kufungua shauri hili.

Walipinga uamuzi wa Baraza Kuu kwa kuwa pamoja na mambo mengine, hawakupewa haki ya kusikilizwa, ambayo ni haki ya msingi.

Waliiomba mahakama; itengue mchakato na uamuzi huo, iamuru CHADEMA kutimiza wajibu wake kisheria kwa kuwapa haki ya kuwasikiliza na itoe zuio kwa Spika na Tume ya Uchaguzi (NEC) kuchukuliwa hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapoamuliwa.

Mbali na CHADEMA kupitia Bodi yake ya Wadhamini, wadaiwa wengine katika shauri hilo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye pia alisimama kwa niaba ya Bunge la Tanzania na NEC.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
15.12.2023

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa kuanzia siku ya **Jumamosi tarehe 16-12-2023 hadi tarehe 19-12-2023** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi,** gari hizo zina namba za usajili: **T 980 EDR / T 877 EAU T 868 DXS / T 881 EAU T 249 EAZ / T 499 DZX**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 24.00** |
| **Upana** | - | **mita 4.70** |
| **Kimo** | - | **mita 5.40** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

117737402

## MCC yarejesha msaada baada ya miaka saba

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa maendeleo nchini wamepongeza uamuzi wa Shirika la Changamoto za Milenia (MCC) kurejesha msaada wa fedha Tanzania baada ya kuusitisha kwa takribani miaka saba.

MCC ilisitisha misaada kwa Tanzania katika miradi mbalimbali ya maendeleo mwaka 2016 kwa kile ilichodai kuwapo ukiukwaji wa sheria katika uchaguzi mkuu Zanzibar. Mara ya mwisho shirika hilo lilitoa msaada wa Dola za Marekani milioni 698 mwaka 2008 ambazo zilitumika hadi mwaka 2013 katika miradi ya kupeleka umeme vijijini.

Aidha, mwaka 2016 MCC ilisema Tanzania haijatimiza viwango vinavyohitajika ili kunufaika na ufadhili, hivyo basi haitapokea msaada wa awamu ya pili ambao ulikuwa wa Dola milioni 472.8.

Taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, ilisema shirika hilo limeichagua Tanzania kuingia katika mpango wa kupata msaada wa fedha zitakazosaidia mabadiliko ya sera na kitaasisi ili kufanikiwa kupata mpango wa 'Compact'.

**WADAU WAPONGEZA**

Ofisa Mkuu Mtendaji wa Taasisi ya Uongozi na Maendeleo ya Ujasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema ujio wa fedha hizo una faida kubwa katika kusaidia ajenda ya maendeleo ya Tanzania.

Alisema Tanzania imetumia fedha nyingi katika maendeleo ya miundombinu, hivyo ufadhili huo utasaidia sekta hiyo na kuokoa fedha za bajeti ambazo sasa zitaelekezwa kwenye masuala mengine muhimu.

"Hii ni ishara kwamba uhusiano wetu na nchi zingine na mashirika ya kimataifa umeimarika. Kwa hiyo haya yalikuwa mafanikio na kitu kizuri kusaidia kwa sababu tuko katika kijiji cha kimataifa," alisema.

Mtafiti Mwandamizi Mstaafu, Prof. Alphonce Kyessi, alisema fedha hizo ni muhimu hasa katika kipindi hikii ambacho nchi inahitaji fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo ikiwamo kutayarisha Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050.

Alisema ili dira hiyo iwe jumuishi inahitaji kukusanya watu kutoka taaluma mbalimbali watoe mawazo yao jambo linalohitaji fedha za kutoka kukamilisha utekelezaji wake.

Alisema makundi hayo yanahitaji kuwezeshwa ili yakae kudadavua na kukubaliana kuhusu vipaumbele vya nchi kwa miaka 25 ya ikiwamo maswala muhimu kama makazi endelevu na nyumba bora kwa kila Mtanzania mijini na vijijini. Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti ya Repoa, Dk.Donald Mmari alisema mchango wa MCC ulikuwa nyongeza muhimu katika maendeleo hasa uboreshaji wa miundombinu, hivyo kurejeshwa kwake kutaongeza kasi ya nchi kufikia malengo iliyojiwekea kimaendeleo.

Alisema kama taifa linaloendelea Tanzania inahitaji ushirikiano wa maendeleo ya kimataifa, kufanya kazi na nchi zilizoendelea zenye nia ya kweli ya kuunga mkono juhudi za uhamishaji kwa kasi na mandhari ya maendeleo ikiwamo kupata teknolojia inayokua.

Pia alisema Tanzania inapiga hatua nzuri katika demokrasia kuliko nchi zingine nyingi barani Afrika na uamuzi wa MCC kusitisha misaada kwa kigezo hicho mwaka 2016 ulikuwa wa bahati mbaya na pengine ungeepukwa kwa uelewa wa kidiplomasia.

**IMF YAMWAGA NOTI**

Wakati huo huo, Bodi ya Utendaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) imekamilisha mapitio ya pili ya Mpango wa Kuongeza Mikopo (ECF) kwa Tanzania, ulioidhinishwa Julai, 2022 kwa ajili ya kupata Dola za Marekani milioni 1,046.4. (Sh. trilioni 2.62)

Taarifa iliyotolewa na taasisi hiyo ilisema kukamilika kwa uhakiki huo kunaruhusu utolewaji wa haraka wa Dola milioni 150.5 (takribani Sh. bilioni 375) na kufanya upatikanaji wa jumla wa Tanzania chini ya mpango huo kufikia karibu Dola milioni 455.3 (sawa Sh. trilioni 1.137).

IMF pia ilisema katika taarifa hiyo kuwa mpango huo unalenga kusaidia ufufuaji wa uchumi, kuhifadhi uthabiti wa jumla wa fedha na kukuza ukuaji endelevu na shirikishi ili kuimarisha mfumo wa sera ya fedha, usimamizi wa sekta ya fedha na kuendeleza mageuzi ya kimuundo.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Thomas Laban ( wa pili kulia), akikabidhi tuzo kwa Prof. Makenya Maboko (kushoto), mzungumzaji mkuu kwenye kongamano la 33 la Wanazuoni wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania lililofanyika katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.**PICHA: MPIGA PICHA WETU.**

## Serikali yabainisha kuwapo ongezeko maambukizi UVIKO-19

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imebainisha kuwa takwimu za ufualitiliaji za Wizara ya Afya zinaonyesha kuwapo kwa ongezeko la maambikizi ya ugonjwa wa UVIKO-19 kutoka watu 37 mwezi Oktoba, mwaka huu hadi 65, Desemba.

Pia, kuna ongezeko la maambukizi ya mafua yanayotokana na influenza kutoka 34 hadi 49.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu, mwenendo huo wa ongezeko la magonjwa hayo ulionekana pia katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Alisema mwaka huo wagonjwa wa UVIKO-19 waliongezeka kutoka 15 mwezi Oktoba hadi 65 mwezi Dsemba, wakati Influenza walikuwa viwili hadi 59 katika kipindi hicho hicho.

"Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa na inaelekeza wataalam katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuendelea kufanya utambuzi kwa njia ya vipimo vya maabara na kutoa matibabu stahiki," alisema na kuongeza:

"Wizara inashauri wananchi kuwahi kwenye vituo vya kutolea huduma wapatapo dalili za magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa zikiwamo mafua, kikohozi, kuwashwa koo, kupumua kwa shida, homa na kuumwa kichwa," alisema Prof. Nagu.

Pia, alishauri wananchi kuzingatia kanuni za afya ikiwamo, kutoshikana mikono ikiwa si lazima kufanya hivyo, kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vipukusi mara kwa mara na kuzingatia usafi binafsi na mazingira.

Mengine alishauri kufunika pua na mdomo wakati wa kukohoa au kupiga chafya pamoja na kuvaa barakoa pale inapohitajika. Sambamba na kupata chanjo kamili ya UVIKO-19 kwa wote ambao hawajachanja au kukamilisha chanjo.

Aliwatoa hofu wananchi, akieleza kuwa serikali inaendelea kufuatilia na kudhibiti magonjwa ya milipuko kwa kupitia mifumo madhubuti iliyopo nchini. Na Wizara itaendelea kutoa taarifa kwa wananchi itakapohitajika kufanya hivyo. Rais wa Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA), Jumanne Baluhya, alisema katika jamii kuna magonjwa mbalimbali na ya mlipuko ndiyo yanayokuwa na madhara zaidi kwakuwa yanawafikia wananchi wakati ambao hawajajiandaa kwa chochote, akieleza kuwa inachokifanya serikali ni kuwakumbusha wananchi kuchukua tahadhari.

"Kutokana na suala hilo serikali inaendelea kusambaza vifaa vya kujikinga vya kutosha kwa watoa huduma za afya ambao wanawahudumia wagonjwa, kwasababu kumpoteza mtaalamu mmoja ni sawa na kuhatarisha watu 10, hivyo tuendelee kuchukua tahadhari tusije tukarudi kwenye sintofahamu iliyopita," alisema Baluhya.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS,

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

TAREHE: 11/12/2023

TAARIFA KWA UMMA

MKURUGENZI WA MANISPAA YA KINONDONI ANAWATAARIFU WANANCHI WOTE KUWA, HIVI KARIBUNI SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, IMEREJESHA KATIKA NGAZI YA HALMASHAURI ULIPAJI WA KODI ZA MAJENGO.

HIVYO, WANANCHI WOTE WENYE MAJENGO NDANI YA MANISPAA YA KINONDONI, WANATAKIWA KUANZA KULIPIA KODI ZAO ZA MAJENGO KUANZIA JANUARI, 2024.

HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA KWA MMILIKI YEYOTE AMBAYE HATOLIPA KODI YA JENGO LAKE.

IMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
MANISPAA YA KINONDONI

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, S.L.P. 31902, 2 Barabara ya Morogoro, 14883 Dar es Salaam
Unaweza pia kuwasiliana nasi kwa Simu: +255 2170173 Nukushi: 2172606, Baruapepe – info@kinondonimc.go.tz



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk Jim Yonazi akipokea msaada wa vitu mbalimbali kutoka Mtandao wa Polisi wanawake (TPF NET), ambao umekabidhiwa na Kamishna wa Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii CP Faustine Shilogile na Kamishna wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu CP Suzan Kaganda, kwa ajili ya waathirika wa maafa ya maporomoko ya matope yaliyotokea Wilaya ya Hanang mkoani Manyara. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Waziri aamua ma-DED wafutiwe barua za onyo

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, ametengua barua za onyo ambazo alielekeza waandikiwe baadhi ya wakurugenzi mkoani Shinyanga.

Alitengua barua hizo jana alipozungumza na watumishi mkoani Shinyanga alipofika kukabidhi magari manne ya sekta kwa afya na kusema uamuzi huo umetokana na utekelezaji mzuri wa miradi ya maendeleo.

Waziri huyo alisema wakurugenzi wamefanya usimamizi mzuri wa fedha za maendeleo, hivyo ameamua kutenga barua za onyo ambazo alikuwa ameelekeza ziandikwe dhidi ya baadhi ya wakurugenzi.

"Kutokana na taarifa ambayo nimeipata hapa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa kwamba wakurugenzi mmejirekebisha na kufanya vizuri katika usimamizi wa miradi ya maendeleo, nimeamua kutengua barua za onyo ambazo nilikuwa nimewapatia baadhi ya wakurugenzi hapa Shinyanga.

"Kwa mkurugenzi ambaye anafanya vizuri, kwangu atakuwa rafiki mzuri. Yule goigoi anayefikiria rushwa nitamwondoa," alionya. Waziri huyo aliwataka wakurugenzi kubuni vyanzo vipya vya mapato. Kila mwaka wanapaswa kubuni vyanzo angalau viwili na kusimamia ukusanyaji mapato. Ndicho kipimo chao.

Aliwataka wakurugenzi kusimamia uandikishaji wanafunzi mwakani na kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ya mradi wa Boost hadi kufikia Desemba 31 mwaka huu uwe umekamilika.

Alionya kuwa mtumishi ambaye hatofanya kazi vyema atamwondoa mara moja na kuweka watu wengine ambao wana nia ya kufanya kazi. Alisema maombi ya kazi ni mengi. Akiwataka watumishi wafanye kazi kwa kushirikiana na kuzungumza lugha moja na kushikamana.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani mwake, alisema ndani ya miaka miwili na nusu ya Rais Samia, wamepokea Sh. trilioni moja za utekelezaji wa miradi. Alisema fedha hizo zimetumika vizuri kwa usimamizi wa wakurugenzi, madiwani, wakuu wa wilaya na wabunge na kufanikiwa kutekelezwa miradi mingi ya maendeleo.

Alishukuru kwa kupatiwa magari manne ya kusaidia usimamizi katika sekta ya afya. Watayatunza na kusimamia matumizi yake.

# Mzazi wa Mtanzania aliyeuawa na Hamas kupelekwa Israel

**Na Halfani Chusi**

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imesema itampeleka Israel baba mzazi wa Joshua Molleli na mwanafamilia mwingine kuungana na Balozi wa Tanzania aliyeko huko kuzungumza na mamlaka za nchi hiyo ili kupata taarifa za ziada kuhusu kifo cha mwanawe.

Novemba 23, mwaka huu huu ilitolewa taarifa kutoka Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali cha wizara hiyo, kwamba Joshua alikuwa ni miongoni mwa vijana wa Kitanzania wapatao 260 waliokwenda Israel kushiriki mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vitendo chini ya Mpango wa Ushirikiano Kati ya Serikali ya Tanzania na Israel.

Hata hivyo, kutokana na machafuko yaliyosababisha mtanzania mwenzake Clemence Mtenga kupoteza maisha, yeye hakuonekana na hakujulikana aliko mpaka ilipotolewa taarifa na serikali yao jana kwamba naye alifariki dunia.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Januari Makamba jana, inabainisha kuwa wamejulishwa na Serikali ya Israel kwamba Joshua Mollel, kijana wa Kitanzania aliyekuwa anasoma Israel, waliyelipoteza mawasiliano yake tangu tarehe 7 Oktoba 2023, ni miongoni mwa waliopoteza maisha.

"Serikali imekuwa inafanya jitihada kubwa kupata taarifa zake tangu wakati huo, aliuawa mara tu baada ya kutekwa na kundi la Hamas mnamo tarehe 7 Oktoba 2023.

"Nimeongea na Mzee Mollel, baba mzazi wa Joshua kuhusu ujumbe huo wa Serikali ya Israel. Tunaendelea na mpango wa awali wa kuwapeleka Mzee Mollel na mwanafamilia mwingine pamoja na Ofisa wa Serikali nchini Israel kuungana na balozi wetu na maofisa waliopo huko, kukutana na kuzungumza na mamlaka za nchi hiyo ili kupata taarifa za ziada.

"Kwa ridhaa ya familia na itakapobidi, tutatoa taarifa za ziada katika siku zijazo," Waziri Januari alisema katika taarifa yake hiyo.

# JKCI yajivunia kubadili valvu za mshipa mkubwa kwa wazee

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema inajivunia mapinduzi kwenye sekta ya afya nchini kutokana na uwekezaji unaoendelea wa vifaa tiba na huduma za ubobezi.

Pia imesema inajivunia Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kubadilisha valvu za mshipa mkubwa wa moyo kwa wazee wenye umri kati ya miaka 75 na 80.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, alipowatembelea wagonjwa watatu JKCI waliobadilishiwa valvu ya mshipa mkubwa wa moyo (TAVI), bila kufungua kifua. Ni huduma ya kwanza nchini na ya pili kwa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara kuitoa.

Alisema hatua hiyo ni baada ya uwekezaji unaoendelea kufanywa katika sekta hiyo, ikiwamo kutengwa Sh. bilioni tano kwa mafunzo ya wataalamu wa huduma bobezi na kibingwa nje ya nchi.

"Mwaka ujao zitatengwa Sh. bilioni 10.9 kwa wataalamu 700 kutoka hospitali tofauti nchini, ikiwamo JKCI kuwasomesha katika huduma bobezi na za kibingwa," alisema Dk. Jingu.

Aliainisha manufaa ya uwekezaji katika sekta hiyo, hasa JKCI ni mapato ya Sh. milioni 920 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka huu kutokana na wagonjwa 3,000 waliotibiwa wakitoka ndani na nje (nchi 20).

"Uwekezaji huu unaokoa maisha, gharama si kwetu tu bali na nchi jirani, pia wapo wanaotoka nje ya bara la Afrika.

"Tutaendelea kuzindua huduma kama hizi, huduma ya TAVI nilipofanya utafiti nimebaini inafanyika Afrika Kusini na hapa Tanzania kwa kusini mwa Jangwa la Sahara," alisema Dk. Jingu.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema watu wazima watatu wenye umri wa kati ya umri wa miaka 75 na 80, wamepatiwa huduma hiyo kwa saa moja na nusu hadi mbili kwa kila mgonjwa na gharama zake ni Sh. milioni 80 kwa mgonjwa.

Awali Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, Dk. Tatizo Waane alisema huduma ya TAVI inapunguza madhara kwa mgonjwa, kwa kuwa hutumia chini ya siku mbili mgonjwa kuruhusiwa.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kutoka Hospitali ya Stancare ya India, Dk. Ashishkumar Mandalay, akiwa na wataalamu wenzake, alisema kutolewa huduma ya TAVI kwa kushirikiana na JKCI, kumewaongezea uzoefu.

Alisema kuwapo vifaa tiba vya kisasa kumefanikisha huduma hiyo, pia mabingwa wa nchini. Ujuzi wao ulisaidia upasuaji huo kufanywa kwa urahisi.

# CCM yampongeza Samia ushawishi kwa vijana

**Na Halfani Chusi**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema Rais Samia Suluhu Hassan ni mfano wa kuigwa kwa vijana wa Afrika, wakiwamo wa kike wanaotaka kuwa mahiri na kujenga ushawishi mkubwa katika maeneo mbalimbali ya uongozi.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Anamringi Macha, alisema hayo juzi alipokuwa akitoa salamu za chama kwa viongozi vijana wanawake kutoka nchi 16 za Afrika, wanaoshiriki Mkutano wa Mwaka wa Taasisi ya Young Women of Africa (YWOA), unaofanyika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha mkoani Pwani.

"Tunapozungumza muda huu kutoka hapa tulipo, kuna idadi kubwa ya wanawake katika nyanja mbalimbali za maisha ambao wamefanikiwa kubadilisha mtazamo na mwonekano wa jamii kuhusu wanawake, katika nchi zao, Afrika na dunia kwa ujumla.

"Wamekuwa mfano wa kuigwa kwa namna ambavyo wameweza kudhihirisha pasipo shaka yoyote kuhusu uwezo na nguvu za mwanamke.

"Kwenye nyanja ya siasa, hapa tunaye Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye umahiri, uimara na uwezo katika uongozi, unatambuliwa na kukubalika duniani kote sasa. Wiki iliyopita tu, Jarida la Forbes limemtaja kuwa ni mmoja wa wanawake 100 wenye nguvu na ushawishi mkubwa duniani," alisema.

Macha alisisitiza umuhimu wa kujiamini kwa kutumia dhana ya uwezo wa mwanamke, kuliko kujikita kwenye udhaifu zaidi, alitolea mfano wa mgombea urais wa Chama cha SWAPO cha Namibia kwenye uchaguzi mkuu wa nchi hiyo mwaka kesho, akisema ni mfano mwingine wa jinsi ambavyo wanawake wanapaswa kubadili mitazamo ya dhana za udhalilishaji.

"Tunapozungumza hapa, wenzetu SWAPO wa Namibia, wanajiandaa na uchaguzi mgombea wao wa urais ni mwanamke. Kwa hiyo nao wanajiandaa kutufuata sisi Tanzania kwa kuwa na Rais mwanamke. Mifano hii tunayo kwenye nyanja zote za maisha sasa, hata zile zinazoendesha dunia, iwe kwenye kisiasa, iwe taaluma, michezo na zingine zote utakazoweza kusema" alisema.

Vilevile alitoa wito kwa viongozi vijana wanawake kutokuwa wanyonge katika kuhakikisha wanatimiza ndoto za mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali katika maisha yao.

# TEC yawanoa walimu mabadiliko mitaala

**Na Carren Mgonja**

BARAZA la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), kupitia Idara ya Elimu kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), wametoa mafunzo kwa walimu wa shule za awali na msingi zinazomilikiwa na kanisa hilo ikiwa ni sehemu ya kuwaandaa kwa mitaala mipya iliyoboreshwa.

Mkuu wa Idara ya Elimu TEC, Sista Joyce Mboya, alisema kwa kuanza, mafunzo hayo yametolewa kwa walimu 150 kutoka shule za kanisa chini ya Jimbo Kuu la Dar es Salaam likihusisha majimbo ya Tanga, Morogoro, Ifakara, Mahenge na Dar es Salaam na yataendelea kwenye majimbo yote nchini.

"Tunatarajia mafunzo kama haya pia yafanyike kwenye majimbo makuu ya Dodoma, Tabora, Mwanza, Mbeya, Songea na Arusha na matarajio hadi kufikia mwishoni mwa Januari, mwakani, walimu wote wawe wameshapata mafunzo haya ili wanapoanza muhula mpya wa masomo wawe tayari wamekwishajua nini kinatakiwa kufanyika kulingana na mabadiliko haya ya mitaala," alisema Sista Mboya.

Akifungua mafunzo hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu wa TEC, Mkurugenzi wa Huduma za Jamii, Padri Paulo Chobo, aliwataka washiriki kujenga umakini kipindi chote cha mafunzo kwa kuzingatia umuhimu wao kama walimu.

"Ni wazi kwamba nia ya serikali kufanya mabadiliko ya elimu ni kuwezesha wanafunzi kupata elimu itakayowajenga katika maisha wanayoendelea baada ya kuhitimu, hivyo ili liweze kufanikiwa, walimu ni nyenzo na watu muhimu kwani wao ndio wanaoshusha elimu hii ya mitaala mipya kwa wanafunzi, hivyo uelewa wenu ndiyo mafanikio ya kile kinacholengwa na serikali," alisema Padri Chobo.

Alisema kanisa limeona ni wakati mwafaka kuwaandaa walimu wake ili kwa kutumia weledi wao na kwa kuongezewa mafunzo hayo ya kuwajengea uwezo kuhusu mitaala mipya, kanisa litaendelea kutunza heshima na sifa yake ya kutoa elimu bora yenye kuzingatia maadili na ufaulu kwa wanafunzi wake.

Mtunza Mitaala kutoka TET, Stephen Mwashihava, alisema ujio wa mafunzo hayo unazidi kuijengea mamlaka hiyo matumaini zaidi kwa shule za kanisa ambazo zimeonyesha nia ya kwenda na kasi ya mabadiliko ya mitaala.

Mwashihava amesema kuwa pamoja na mambo mengine, katika mafunzo hayo washiriki watapata nafasi ya kupewa mbinu juu ya uchambuzi wa mitaala hiyo mipya katika ngazi ya shule za awali, shule za msingi kwa kila darasa na kuchambua mihutasari ya kila somo, lakini zaidi kuwapa washiriki mbinu za ufundishaji na maandalizi ya somo na jinsi ya kupima uelewa wa wanafunzi.

Mabadiliko ya mitaala ya elimu yametokana na agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alilolitoa Aprili 22, 2021 jijini Dodoma, likiwaelekeza Wizara ya Elimu kutoa elimu inayowajengea wanafunzi uwezo wa kujiajiri na hata kuingia kwenye soko la ajira baada ya kuhitimu masomo yao.


DERM group

25th Anniversary Of PROFESSIONAL EXCELLENCE

**Derm Group (T) Ltd and its subsidiaries** wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices will be closed during the festive season with effect from Friday **22nd December 2023.**

**Business will resume on Monday 8th January 2024.**

Our site operations and regional offices in **Dodoma, Geita, Songwe, Tanga, Mbeya, Mtwara, Kigoma and Zanzibar** shall not be affected by this closure.

Any inconveniences caused is highly regretted.
We would like to thank all our clients and business partners in general for their continued patronage of our services throughout the year.

"We wish you all a Merry Christmas and prosperous, productive and innovative 2024".



SKYLINE PROPERTIES LTD

Derm Elevators

dermgrouptz
info@derm.co.tz
www.derm.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wajifunze kuchukua hatua katika kutatua mambo

**JANUARI** kila mwaka, wanafunzi waliomaliza darasa la saba huanza masomo yao ya sekondari, wengi katika shule za umma na wachache zile za binafsi na mashirika ya dini.

Matokeo ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi yameshatoka na hivi sasa kinachofuata ni mchakato wa kuwapangia shule huku wale wanaojiunga na shule binafsi wameshafanya mitihani kwenye shule husika na wengi wameshapangwa. Pia baadhi ya shule binafsi zinaendelea kutangaza nafasi za kujiunga kwa wale ambao wanatamani kusoma kwenye shule hizo lakini kwa sababu mbalimbali walikosa nafasi kutokana na idadi na ushindani mkali katika shule hizo.

Suala la kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za sekondari za serikali linafahamika miaka yote kwamba ifikapo Januari kila mwaka ni lazima jambo hilo lifanyike. Kwa wale ambao hushindwa kujiunga kwa muda huo, hupewa muda hadi mwishoni mwa Februari wawe wameshafanya hivyo.

Katika miaka ya karibuni, kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, wengi katika shule za kata na wengine wachache shule za vipaji maalum au zile za bweni.

Pamoja na ongezeko la ufaulu na idadi ya wanaochaguliwa kila mwaka, changamoto kubwa imekuwa ukosefu wa miundombinu ya kutosha, vikiwamo vyumba vya madarasa. Hatua hiyo husababisha serikali kuanzia ngazi ya wilaya kuchukua hatua za kukamilisha miundombinu hiyo huku ikiwashirikisha wananchi wanaoishi au kutoka maeneo husika.

Awali, tatizo hilo lilionekana kama la dharura takriban miaka mitano hadi saba iliyopita lakini sasa linaonekana kuwa la kawaida kutokana na kujirudia kila mwaka. Hali hiyo imeonekana hivyo baada ya juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, kutoa kauli kuwa wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa ambao hawatakamilisha miradi ya maendeleo, ikiwamo ya elimu na afya, ifikapo Desemba 31, mwaka huu, watachukuliwa hatua.

Katika kauli yake hiyo, Mchengerwa alisema hatasita kuwasemea kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili watenguliwe kwenye nafasi zao kwa kushindwa kukamilisha miradi hiyo kwa wakati huku wananchi wakisubiri ikamilike na kupata huduma.

Waziri Mchengerwa ameibua maswali kadhaa kutokana na kauli hiyo. Miongoni mwa maswali hayo ni kwa nini arejee kauli kama hiyo ilhali zikiwa zimebaki chini ya siku 31 kabla ya wanafunzi kujiunga na kidato cha kwanza? Kwa nini kauli hiyo ya kuwatangazia 'kiama' wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa na kuwatishia kutenguliwa itolewe sasa badala ya miezi miwili au mitatu iliyopita?

Kauli hiyo ya Mchengerwa, Waziri aliyepewa dhamana katika masuala ya elimu ya msingi hadi sekondari ambazo ziko chini ya halmashauri anazoziongoza, kwa mtazamo yakinifu, haikupaswa kutolewa juzi kama ilivyofanyika. Kabla ya kufanya hivyo, ofisi yake ilitakiwa kuwa imekusanya taarifa za maendeleo ya ujenzi wa miundombinu hiyo na kuwa na majawabu thabiti angalau Septemba, mwaka huu, na kubaini changamoto zilizopo, vinginevyo, kauli hiyo inaweza kuonekana ya kisiasa zaidi badala ya uhalisia wa mambo.

Ni wazi kwamba serikali ina mipango ambayo utekelezaji wake ni wa muda maalum, hivyo haikupaswa kwa kiongozi wa ngazi ya Waziri kusema wasiotekeleza ujenzi wa miundombinu hiyo atawachongea kwa Rais ili waondolewe katika nafasi zao.

Alichopaswa kukifanya, kwa kiongozi ambaye ana utashi wa kufanikisha jambo, ni kubaini changamoto na kuchukua hatua za kuzitatua kabla ya kutoa tamko kama hilo.

Ni vyema viongozi wetu wakawa wafuatiliaji wa mambo ikiwamo utekelezaji wa miundombinu ya huduma za afya kama elimu na afya kisha kuchukua hatua mapema badala ya kutoa kauli za kuwaweka roho juu wateule wenzao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Msimu kilimo ndio huo, wanakonasa wakulima ni mbegu kuwa bei juu

Na Halfani Chusi

**MSIMU** wa kilimo umefika, wakulima tukiwa na angalizo, ili kuweza kupata kipato kikubwa kulingana na eneo, lazima kutumia mbegu kuzalisha nafaka na sio nafaka kuigeuza mbegu.

Nilihuduhuria semina iliyowakutanisha wataalamu wa kilimo. Moja ya hoja iliyopamba moto kwenye ukumbi huo, ilikuwa wakulima wengi wanapata kipato kidogo, kwa sababu hawatumii mbegu kuzalisha chakula bali wanatumia nafaka.

Wataalamu hao walisema, mtu anapotumia mbegu ya dukani kwenye kilimo, anakuwa kajiweka katika asilimia 40 ya kupata kipato kikubwa, lakini destuli za wakulima wengi nchini na hata kupata kipato kidogo ni kutokana na wengi wao kugeuza nafaka kuwa mbegu.

Ni utaratibu wa kawaida tu, unakuta mkulima wa mahindi katumia aliyoyavuna kama mbegu, jambo ambalo walilikosa wataalamu hao wakidai linamfanya mkulima apate kipato kidogo.

Vilevile, nimeshuhudia wakulima wa nyanya nao wanapovuna wanakuwa na mbegu ambayo wanakuja tena kuitumia kwenye msimu uanaofuata wa kilimo, jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa wataalamu.

Ukweli dhahiri, ili kuwa na kipato bora, pia mafanikio makubwa katika kilimo, kunapaswa mkulima anunue mbegu kutoka dukani na sio kutumia mbegu inayotokana na mazao anayovuna, na itasaidia kupata uhakika wa kipato kikubwa na kujiondoa katika kilimo cha kujikimu. Ndiyo namna ya kufikia azma ya kilimo cha biashara.

Unapojaribu kuwadodosa wakulima, nini kinawakwamisha kufikia hatua hiyo, huitaja gharama ya mbegu isiyotokana na nafaka yao kuwa juu.

Ninachokiona ni ukweli. Ukiangalia kwa mfano mbegu ya nyanya ya dukani, inauzwa kwa gharama kubwa sana na ili ulime ekari moja, ni lazima mkulima awe na mtaji wa shilingi laki tatu za kununua mbegu pekee.

Lakini ile ya kukamua, ambayo ndio inakosolewa na wataalamnu wa kilimo. ukipimiwa ni ya shilingi elfu 50 pekee,i unaweza kulima zaidi ya ekari moja. Hiyo inaonyesha dhahiri kwamba, wakulima wanashindwa kwa sababu ya bei ya juu ya mbegu.

Ninachoishauri serikali na wadau wa kilimo, waweke utaratibu mzuri wa kuwakopesha wakulima mbegu bora, ili baaada ya mavuno waweze kurejesha fedha zao. Hiyo naamini itawasaidia sana kwa wakulima wasio na uwezo wa kununua mbegu bora dukani.

Pia, kuna haja ya kuwatembelea wanapokuwa shambani kuona maendeleo ya mazao yao na hata kuwasaidia pale wanapoona wanakwama. Kuna uwezekanao kwao wakapata kipato kikubwa, watakapopata mbolea na dawa za tiba kwa mimea.

Pia, wapate elimu sahihi za kutunza mazao, pamoja na kuwasaidia namna ya kupata soko kutokana na kile wanachokipata kutoka shambani.

Pamoja na kwamba serikali imekua ikitoa mikopo kwa wakulima lakini bado kuna makundi hayaguswi moja kwa moja, hasa kwa wakulima walioko vijijini, kwa kuwa wengi wao hawajajiunga katika vyama vya ushirika lakini kuna haja ya kuangalia namna ya kuweza kuyafikia makundi hayo.

Ninashauri, pia serikali iangalie namna ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji vijijini kwenye maeneo ambako kuna ardhi kubwa, lakini hakuna umwagiliaji, kwa sababu eneo lenye umwagiliaji, ni rahisi mkulima kupata kipato kikubwa na sio cha kubahatisha kama kutegemea mvua.

Unakuta kijiji kipo sehemu fulani kina ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, lakini hakuna maji kwaajili ya umwagiliaji kwa hiyo wanalazimika kutumia kilimo cha msimu mmoja tu yaani kile cha kutegemea mvua jambo amabalo linarudisha nyuma juhudi za kuinua sekta ya kilimo na uchumi wa nchi.

# Watumishi waondolewa hofu utendaji wa mfumo wa HRA

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete amesema Mfumo wa Mahitaji ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma (HRA) hauna lengo la kumwondoa kazini au kuwaonea watumishi wa umma, hivyo hawana sababu ya kuwa na hofu nao.

Ridhiwani aliyasema hayo jana wakati wa kufunga mafunzo ya siku tatu kwa watumishi wa umma kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Shirika la Masoko Kariakoo na Bodi ya Sukari Tanzania yaliyofanyika MOI, jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo la mfumo huo ni kuiwezesha kupima utendaji wa watumishi wake kwa njia rahisi na kuongeza ufanisi wenye tija kazini.

"Mfumo huu hauna lengo la kukomoa watu, tutakuwa na utumishi wa umma unaotimiza majukumu, utawezesha kupanga utumishi wenye tija, huna sababu ya kuhofia," alisema.

Aliongeza kuwa mifumo hiyo inakwenda kuonesha wapi penye upungufu ili paboreshwe, akipongeza MOI kwa kutoa huduma bora kwa Watanzania na kuitaka kuendelea na kasi hiyo kwa maslahi ya umma.

"MOI inaendelea kuwa bora. Hii yote ni juhudi zako Prof. Makubi na timu yako, hongera sana, tunahitaji utumishi wenye tija," alipongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Prof. Abel Makubi, akimkaribisha naibu waziri huyo, alimpongeza kwa kutembelea taasisi hiyo mara kwa mara na kwamba hatua hiyo inaongeza ari kwa watumishi kufanya kazi kwa uma-



Baadhi ya wanachama wenye matatizo ya uti wa mgongo (Spinal cord injury) ambao ni wanufaika wa miradi mbalimbali inayofanywa na shirika lisilo la kiserikali la Songambele Initiative wakimsikiliza Mkurugenzi wa shirika hilo, Faustina Urassa (hayuko pichani) katika Mkutano Mkuu Maalumu wa nne (AGM) wa shirika uliofanyika jana mjini Moshi kujadili changamoto wanazopitia na namna ya kukabiliana nazo ikiwamo utoaji wa vitimwendo kwa watu wenye uhitaji. **PICHA: JAMES LANKA**

# Waziri, shirika wakabidhi misaada waathirika maporomoko Hanang

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo amewapatia misaada mbalimbali waathirika wa mafuriko na maporomoko ya tope yaliyotokea Katesh, wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Dk. Jafo alitoa misaada hiyo wakati wa ziara yake ya kuwafariji waathirika wa mafuriko wanaopewa makazi ya muda katika Shule ya Sekondari Katesh.

Waziri huyo pia alikagua athari za maafa hayo yaliyotokea Desembea 3, mwaka huu kutokana na kumeguka kwa sehemu ya Mlima Hanang.

Akizungumza na Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janet Mayanja pamoja na watumishi mbalimbali wa serikali wanaotoa huduma kwa wathirika, Dk. Jafo alisema Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), imeanza kufanya tathmini katika eneo hilo.

Alisema tathmini inafanyika kuangalia ni wapi panafaa kujengwa makazi na maeneo ya huduma za kijamii ikiwamo soko ambalo limeathiriwa na hivyo kuepusha madhara yasitokee wakati mwingine.

"Mimi binafsi na familia yangu nimejitolea misaada ikiwamo mavazi haya na vifaa hivi ili kuwafariji waathirika wa maafa haya na ninawaomba tuwe na subiri wakati serikali inaendelea kuhakikisha mnarudi katika hali mliyokuwa nayo zamani," alisema.

Waziri Jafo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa kuweka nguvu ya kutosha kuhakikisha kila Mtanzania anapata stahiki huduma.

Katika ziara hiyo, Dk. Jafo alifuatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC, Prof. Esnat Chaggu na Mkurugenzi wa Utafiti wa Mazingira wa baraza hilo, Dk. Menan Jangu.

Shirika la WaterAid Tanzania (WAT) nalo limetoa msaada wenye thamani ya Sh. milioni 54.87 kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa wilaya ya Hanang waliokumbwa na maporomoko ya ardhi.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika hilo, Anna Mzinga, alisema wameguswa na tukio hilo na wamekabidhi vifa vitakavyosaidia katika kipindi hiki cha dharura.

Alisema WaterAid Tanzania ni wadau wa maendeleo nchini, wamepokea kwa masikitiko taarifa ya janga hilo na kuamua kutoa msaada unaojumuisha huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi vyenye thamani ya Sh. milioni 39.875. Vifaa hivyo ni vyoo vitatu vya dharura na bafu katika kambi za waathirika.

"Dawa za kusafisha vyoo katoni 50, sabuni za kunawia mikono katoni 100, mifagio na brashi kwa ajili ya usafi pisi 50, matangi sita ya kuhifadhia maji ya kunywa ya lita 2,000 na dawa za kutibu maji kilo 225, matangi makubwa sita ya kunawia mikono yenye ukubwa wa lita 1,000 zenye bomba sita za kunawia mikono kila moja," alifafanua.

Pia alisema WaterAid Tanzania inachangia Sh. milioni 15 kama fedha za dharura kushughulikia mahitaji mengine muhimu ya waathirika wa janga hilo kwenye vituo vya makambi. Mkuu wa Wilaya ya Hanang, Janet, alishukuru kwa msaada huo.

TAARIFA YA MAELEZO

Kwa mujibu wa Mobhare Matinyi, Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, hadi juzi, maporomoko hayo yalikuwa yamesababisha vifo vya watu 89.

*Imeandaliwa na Beatrice Shayo na Robert Hokororo ( HANANG)

# Kanali Laban: Mabadiliko Sera ya Elimu yatakuwa na tija kiuchumi

**Na Miraji Msala**

MABORESHO ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 yanalenga kuifanya elimu itakayotolewa nchini kukidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, alitoa kauli hiyo juzi alipohudhuria Kongamano la 33 la Wanazuoni wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) lililofanyika mjini Songea ambako alikuwa mgeni rasmi.

"Maboresho haya yanalenga kujibu maswali yote kuhusu ajira. Yamekuja na suluhisho la namna changamoto za utungaji mitaala na namna sahihi ya uandaaji wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu ili watambue nafasi zao na namna ambavyo watashiriki katika uzalishaji mali," alisema Kanali Laban.

Makamu Mkuu wa OUT, Prof. Elifas Bisanda, alisema lugha si kikwazo kwa mitaala mipya kwa kuwa kinachotakiwa ni ujuzi na uzoefu wa walimu ambao watautoa kwa wanafunzi.

"Lugha ya kufundishia si tatizo kwa watoto, badala yake ni walimu wanaofundisha kwa kutumia Kiswahili badala ya Kiingereza ambayo ndiyo lugha ya kufundishia kuanzia elimu ya sekondari.

"Kimsingi, walimu hao wanatakiwa wawe na uwezo wa kutoa ujuzi kwa lugha husika na wanafunzi wataelewa na kupata ujuzi pale mwalimu anapokuwa mahiri katika lugha ya kufundishia," alisema Prof. Bisanda.

Prof. Makenya Maboko wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambaye alikuwa mzungumzaji mkuu, alisema kuwa wakati umefika kwa Tanzania kubadilisha mitaala yake kupitia sera.

Msomi huyo alisema nchi inapaswa kuitekeleza mitaala hiyo kupitia elimu ujuzi kuanzia ngazi za chini ambayo itaamua mustakabali wa wanafunzi baada ya kumaliza kiwango fulani cha elimu. "Kupitia mtaala mpya wa elimu na mafunzo, itatakiwa muundo mpya utakaoimarisha upatikanaji maarifa, ujuzi na mitazamo itakayozingatia ajira na kujiajiri.

"Uanzishwaji wa programu utakwenda kwa karibu zaidi na mahitaji ya soko la ajira na fursa za kiuchumi nchini," alisema Prof. Maboko. Mhitimu wa Shahada ya Umahiri katika Usimamizi wa Miradi, Dk. Malneste James, aliipongeza serikali kwa kuleta mabadiliko ya Sera ya Elimu, akisisitiza yamefanyika wakati mwafaka.

Alisema anamini jamii itashuhudia mabadiliko makubwa kielimu nchini kutokana na mabadiliko hayo ya kisera.

Kongamano hilo lilikutanisha wasomi hao kwa lengo la kujadili mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 yanayoanza kutekelezwa Januari 8 mwakani.

# MSCL kujenga meli ya mizigo na abiria kwenda Comoro, Shelisheli

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KAMPUNI ya Huduma za Meli (MSCL) imesema iko katika mipango ya kukarabati meli 13 na kujenga meli mpya tisa ifikapo mwaka 2025 kwa lengo la kukamata masoko ya kusafirisha abiria na mizigo katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia na Congo (DRC), Uganda, visiwa vya Comoro na Shelisheli.

Ofisini kwake jijini Mwanza jana, Mkurugenzi Mkuu wa MSCL, Eric Hamissi alisema kuanzisha safari za kwenda visiwa vya Comoro na Shelisheli ni moja ya mipango mikubwa ambayo kampuni imepanga kutekeleza ili kusafirisha abiria na mizigo kwenda nchi hizo.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika kwa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), mizigo kutoka Tanzania itasafirishwa kwa urahisi mpaka Sudan Kusini.

Mkurugenzi Hamissi alibainisha kuwa mpaka kufikia mwaka 2017, MSCL ilikuwa na meli tano; MV. Umoja, MV. Liemba, MV. Clarias, MV. Sangara na MV. Songea ambazo zilizokuwa zinatoa huduma, katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

"Mpaka kufika mwaka huu wa 2023, MSCL inamiliki meli 17. Kati yake, tisa zipo katika Ziwa Victoria, tatu na boti moja katika Ziwa Tanganyika na tano Ziwa Nyasa," alifafanua.

Alisema kwa sasa MSCL inatoa huduma katika visiwa vya Ukerewe, Gana na Godziba kwa kutumia meli za MV. Butiama na MV. Clarias.

Pia kujiunga kwenye taasisi zinazowakutanisha wadau mbalimbali wa biashara, mfano TPSF. Lengo kuu ni kuendelea kupata wateja wa kutumia meli zetu kusafiri na kusafirisha mizigo ndani na nje ya Tanzania.

Kuhusu mafanikio yaliyopatikana toka kuanza rasmi kutoa huduma mwaka 1997, Mkurugenzi huyo alisema:

"Katika awamu ya kwanza ya mpango wa kufufua huduma za usafiri katika maziwa makuu kupitia MSCL, serikali ilitenga zaidi ya Sh. bilioni 200 kwa ajili ya utekelezaji miradi mikubwa minne katika Ziwa Victoria.

"Miradi hiyo ni ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza 'Hapa Kazi Tu', yenye uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria ambayo imefikia asilimia 92, kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 107 na kutekelezwa na mzabuni GAS Entec."

Alisema ukarabati wa meli za MV. Victoria na ukarabati wa meli ya MV. Butiama ulikamilika mwezi Aprili 2020 na meli hizo zinaendelea kutoa huduma katika Ziwa Victoria.

"Miradi yote miwili ilikamilika kwa gharama ya Sh. bilioni 27.6. Kati yake, Sh. bilioni 22.7 ni kwa ajili ya ukarabati wa MV. Victoria 'Hapa Kazi Tu' na Sh. bilioni 4.9 ni kwa ajili ya ukarabati wa meli ya MV. Butiama.

"Miradi hiyo imetekelezwa na mzabuni KTMI Co. Ltd kutoka Korea Kusini kwa kushirikiana na kampuni ya Yuko's Enterprise (EA) ya Tanzania," alisema Mkurugenzi Hamissi," alifafanua.

Aliendelea kuelezea kuwa ukarabati wa meli ya kubeba mabehewa (Wagon Ferry) ya MV. Umoja unaotekelezwa na kampuni ya SM SOLUTION CO. LTD ya Korea Kusini, ulikamilika mwezi Septemba mwaka huu. Ni meli iliyokarabatiwa kwa Dola za Marekani 8,422,840 (Sh. bilioni 19.811).

Alisisitiza kuwa MSCL katika kutekeleza miradi ya ukarabati wa meli chakavu, kwa sasa inatekeleza miradi ya ujenzi wa meli ya MV. Mwanza katika Ziwa Victoria, ukarabati umefikia asilimia 92.

Miradi mingine aliyosema inaendela na utekelezwaji ni pamoja na ukarabati wa meli ya MV Liemba katika Ziwa Tanganyika, tayari mkataba umeishatiwa saini kwa ajili ya utekelezaji.

Alibainisha baadhi ya mikataba ambayo MSCL imeingiana kwa mwaka 2023 ni pamoja na mkataba wa ujenzi wa karakana ya kujengea meli katika Ziwa Tanganyika. Itakuwa na eneo lenye urefu wa mita 188 na upana wa mita 140 na itakuwa na ukubwa wa mita 55,000 za mraba.




Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Ridhiwani Kikwete akiwa ameongozana na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili Prof. Abel Makubi wakati alipotembelea taasisi hiyo mara baada ya kufungua mafunzo kwa watumishi wa umma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahafali chuo kikuu yaanika fursa, changamoto za Songea

**Na Vincent Mpepo,** OUT

KUFANYIKA kwa mahafali ya 42 ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) mkoa wa Ruvuma, hususani katika makao makuu ya mkoa wilayani Songea, kumeanika changamoto na fursa kadhaa ambazo zina athari chanya na hasi kiuchumi katika mkoa huo.

Wageni waliohudhuria mahafali hayo wakiwamo wahitimu, wafanyakazi na ndugu zao katika mahafali hiyo ya 42 ya OUT, wamebainisha fursa na changamoto za wilaya ya Songea.

Mhadhiri Msaidizi wa OUT, Yusuph Manning alisema kuna changamoto ya upatikanaji huduma za malazi (hoteli na nyumba za kulala wageni), lakini akakiri kuridhishwa na miundombinu ya barabara za mji huo.

"Nilisafiri kwa pikipiki, nikizifikia zaidi ya hoteli na nyumba za kulala wageni 10 bila mafanikio," alisema.

Manning alisema ubora wa miundombinu ya barabara na huduma za maji na umeme ni mambo yanayoupa sifa njema mkoa huo.

Hata hivyo, mhadhiri huyo alisema kulihitajika kufanya maandalizi mapema ili kuwa na uhakika wa kupata chumba cha kulala kwa mgeni aliyehitaji huduma hiyo wakati wa mahafali hayo.

Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Mawasiliano ya Umma, Angella Michael, pia alisema kuna changamoto ya uhaba wa hoteli na nyumba za wageni zinazokidhi vigezo, suala analolinyooshea kidole linaweza kurudisha nyuma sekta ya utalii.

Alisema huduma kwa mteja ni jambo ambalo limekuwa ni shida nyingine alipoingia mkoani Ruvuma. Bado watoa huduma wana lugha mbovu na ucheleweshaji huduma kwa wateja, jambo ambalo halina afya kibiashara," alilalama Angella.

Mwendesha pikipiki, Julius Mapunda wa Bombambili mjini Songea, alisema anatamani kila mwaka chuo hicho kije kwa shughuli za mahafali kwa kuwa amepata kipato cha ziada kutokana na idadi kubwa ya abria aliowapatia huduma.

"Kwa siku mbili hizi mapato yamekuwa ya kuridhisha kutokana na ongezeko la idadi niliowabeba", alisema Mapunda.

Mhitimu wa Stashada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii kutoka Mtwara, William Syekeye, alisema anashukuru uongozi wa chuo kwa kupeleka mahafali mkoani Ruvuma kwa kuwa kunasadia kuona maeneo mengine kama sehemu ya utalii na kujifunza.

"Songea kuna ya hewa nzuri na gharama za maisha ni rafiki hususani kwenye vyakula kulinganisha na mikoa ya Lindi na Mtwara," alisema Syekeye.

Mfanyakazi wa OUT, Sara Abdi, alisema mahafali ya chuo kikuu, hasa cha kwao ambacho hufanya mahafali kwa kuchagua mkoa kila mwaka, yanakuwa na changamoto, hasa kwenye maandalizi ya chuo.

Alisema safari hii maandalizi yao hayakuwa mazuri, suala lililosababisha kupata changamoto za usafiri na huduma za malazi mkoani Ruvuma.

# Wilaya yapatiwa vifaa kwa ajili ya wajawazito

**Na Mwandishi Wetu,** KIGAMBONI

VIFAA 750 vya kujifungulia vyenye thamani ya Sh. milioni 15.3 vimekabidhiwa kwa uongozi wa wilaya ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam kwa lengo la kuinua afya ya uzazi katika wilaya hiyo.

Vifaa hivyo vilivyotolewa na Benki ya NMB, ni pamoja na pamba kubwa, mpira ya kuzuia uchafu (disposable mackintosh), taulo za kike za wazazi, nyembe za kupasulia, vibana kitovu vya watoto, nguo za watoto, mabomba ya sindano na nyuzi za kushonea.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi msaada huo iliyofanyika Kigamboni jana, Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Dismas Prosper alisema kupitia msaada huo, wanakusudia kuunga mkono juhudi za serikali za kutoa huduma bora za afya ya uzazi huku akisisitiza kuwa msaada huo utachangia ustawi wa watu binafsi, familia na jamii ndani ya wilaya hiyo.

Prosper alibainisha kuwa benki hiyo imeipa sekta ya afya kipaumbele kikubwa kwenye mkakati kabambe wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSI), ikiamini kuwa afya bora ni chachu ya maendeleo endelevu.

"Benki kwa miaka saba sasa imekuwa inatenga asilimia moja ya faida baada ya kodi (PAT) kufadhili mipango mbalimbali ya maendeleo nchini kama sehemu ya dhamira yetu ya kusaidia maendeleo endelevu katika maeneo ambayo benki yetu inafanya kazi.

"Leo (jana), tuna furaha kukabidhi vifaa vya kujifungulia vyenye thamani ya Sh. milioni 15.3 na tunaamini juhudi zetu zitasaidia sana kuokoa maisha ya wajawazito na watoto wao wachanga," alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigamboni, Pendo Mahalu, wakati wa hafla hiyo, alisema wilaya yake mapema mwaka huu ilifanya tathmini ya mahitaji kwa mwaka iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, na kubaini kuwa wilaya hiyo inahitaji vifaa takribani 8,500 vya kujifungulia kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia wajawazito na watoto wao wachanga.

Alisisitiza kwamba msaada uliotolewa na benki hiyo, umekuja wakati mwafaka na kuihakikishia benki kuwa wilaya yake itatumia ipasavyo vifaa hivyo vilivyotolewa kwa manufaa ya wajawazito wote wenye uhitaji.

"Afya bora inahitaji utoaji huduma za afya kwa wakati na kwa ufanisi. Tunashukuru sana kwa msaada huu na tunaamini vifaa hivi vya kujifungulia vilivyotolewa vitasaidia kuweka tabasamu kwa kinamama wengi ambao mara nyingi wanalazimika kuingia gharama za ziada ili kununua vifaa hivi muhimu," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Kigamboni, Dk. Mohammed Mnyau. alisema msaada huo ni ukombozi mkubwa kwa wajawazito wilayani Kigamboni kwa kuwa vifaa vya kujifungulia ni gharama na kuishukuru benki hiyo kwa mchango wake.

"Wakati mwingine ukosefu wa vifaa vya kujifungulia unasababisha ucheleweshaji wa utoaji huduma usio wa lazima. Tunaamini kuwa baada ya kupokea vifaa hivi kutoka Benki ya NMB sasa tutawezesha kutoa huduma za papohapo kwa wanawake wajawazito wenye uhitaji.

"Kwa wastani, hospitali yetu inapokea kati ya wajawazito 5,000-10,000 kila mwaka," Dk. Mnyau alisema.






Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, akizindua kitabu cha Mwongozo wa Mfuko wa Wakfu (SDTF), wa maendeleo ya wadau wa walipakodi wa zao la mkonge juzi wakati alipofungua mkutano wa nne wa wadau wa zao hilo wilayani Korogwe, mkoani Tanga, kulia ni Mkurugenzi wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona na kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Bashe awaweka viongozi njia panda

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema viongozi waliopewa dhamana ya kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika halmashauri wanamwangusha kwa kukumbuka eneo la kilimo wakati wa kukusanya mapato ya serikali. Bashe ametahadharisha kuwa hatari anayoiona katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga ni kupuuzwa kwa maelekezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Akizungumza juzi katika mkutano wa nne wa wadau wa Sekta ya Mkonge, ulioambatana na uzinduzi wa Mfuko wa Wakfu (SDTF) kwa Maendeleo ya Walipakodi wa Sekta ya Mkonge, Bashe alisema kuwa:

“Kwa Wilaya ya Muheza, mimi nikuombe Mkuu wa Mkoa (Tanga), wakati Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anatoa maelekezo ulikuwepo. Mashamba yale yalirudishwa halmashauri kwa ajili ya kilimo cha mkonge na siyo kugawana viwanja.

“Hatari kubwa ninayoiona ni viongozi tuliopewa dhamana ya kumsaidia Rais katika ngazi ya halmashauri tunakumbuka eneo la kilimo wakati wa kukusanya ushuru, tuna tatizo kubwa la kujadili bila kujadili umasikini, mkuu wa mkoa mkalisimamie suala hili.

Katika baadhi ya wilaya ambazo zimepata tatizo la wananchi kukosa mashamba yaliyochukuliwa na serikali na kukabidhiwa kwa halmashauri ni Muheza na Mkinga. “ Mfano leo, asilimia kubwa ya mapato kwa Wilaya ya Mkinga inatokana na samaki, siku wavuvi wakaamua kuweka pembeni boti zao hawaendi kuvua, hakuna mapato.”

Mkuruenzi Mkuu wa Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Saddy Kambona, alisema wakati anakabidhiwa ofisi mwaka 2019, uzalishaji ulikuwa wastani wa tani 36,000, lakini kwa juhudi za serikali umeongezeka na kufikia tani 48,000 hadi mwaka 2022.

“Matarajio yetu ni kuongeza uzalishaji kufikia tani 60,000, na tulivyotathimini uzalisaji wetu mpaka kufikia nusu ya mwaka, tayari tumezalisha tani 34,000. Hivi sasa tunaona kabisa tunakimbilia lengo la serikali la kuzalisha tani 120,000 ifikapo mwaka 2025 /26,” alisema.

Alisema kwa sasa soko la zao hilo limeimarika na kuongezeka kwa wakulima waliojiunga kwenye Vyama vya Ushirika wa Kilimo (AMCOS) katika Wilaya ya Korogwe. AMCOS hizo ni Magunga, Mwelya, Hale, Mgombezi na Magoma.

# Waziri aagiza watendaji goigoi watimuliwe

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Jamal Katundu ameagizwa kuanza kuwawajibisha watendaji wa wizara hiyo wanaofanya kazi kwa mazoea kwa lengo la kuvuruga mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Agizo hilo lilitolewa na Waziri wa Wizara hiyo, Juma Awesu jijini Arusha jana wakati akishiriki mkutano wa kutoa maoni ya mapendekezo ya Rasimu ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002, Toleo la Mwaka 2023 na Mpango Mkakati wa Wizara hiyo.

Awesu alisema licha ya mafanikio mengi yaliyofikiwa, bado kuna watendaji baadhi ya maeneo lazima wakubali kubadilika na kusimama kama kiongozi kwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Alitoa mfano wa baadhi ya maeneo Mkoa wa Mbeya kuwa baadhi ya watendaji wamepelekewa zaidi ya Shilingi milioni 300 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji na kuamua kugawana.

“Katibu Mkuu chukulia hatua wote wanaokwamisha miradi yetu au wanaofanya kazi kwa mazoea usionee mtu haya, ukicheka na nyenyere atakung'ata kwenye makwapa,” alisema na kuongeza kuwa:

“Ni lazima watendaji, msimame katika nafasi zenu za kazi na mtoe taarifa kwa wakati sehemu sahihi.”

Alisema siku za nyuma kulikuwa na miradi 177 kichefuchefu, ambayo ilimlazimu kuweka nguvu za pamoja na wadau wa sekta ili kuhakikisha inakamilika kabla ya kuanza miradi mipya.

“Ni lazima wizara yetu tukubali kubadilika ili kuruhusu kupata mawazo ya watu binafsi. Zipo hoteli kubwa wanatumia maji na viwanda vikubwa vinatumia maji hawana mita za maji.

...ninawaomba watendaji hili eneo linahitaji uzalendo, ushirikishwaji na lazima tushirikishe wadau wetu wa maendelo ili tufanye mageuzi makubwa katika sekta yetu ya maji,” alisema.

Profesa Katundu, alisema katika kikao hicho cha siku mbili, wadau hao watajadiliana masuala mbalimbali kuhusu sekta hiyo ya maji fursa, changamoto na rasimu ya sera hiyo.

# Mwigulu ataka wabobezi wafanye ununuzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba amemtaka Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kushirikiana na Bodi ya Wataalamu ya Wanunuzi na Ugavi (PSPTB) kuhakikisha shughuli za ununuzi na ugavi zinafanywa na watu wenye sifa.

Akizungumza jana katika ufunguzi wa kongamano la 14 la mwaka la wataalamu wa ununuzi na ugavi, Waziri Nchemba, aliwataka kuzingatia maadili na sheria ili wafanye kazi kwa weledi na kusimamia miradi ya sekta binafsi na umma.

“Mnasimamia miradi mingi ya kimkakati ya sekta binafsi na umma ni lazima nyie bodi kushirikiana na wizara na hili nakuagiza katibu mkuu wangu kuhakikisha linatekelezeka ili kuleta ufanisi zaidi katika usimamizi wa miradi mnayosimamia,” alisema.

Alisema lengo la kongamano hilo kuangalia jinsi ya kupunguza changamoto zilizopo katika fani hiyo pamoja na kubadilishana uzoefu katika sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi wa miradi inayotekelez

Hata hivyo, alisema hafurahishwi kusikia bado kuna watu wasio na sifa na wanaendelea kufanya kazi ndani ya taaluma hiyo na kusababisha kuonekana haina manufaa kwa nchi.

Alisema ni muhimu wakazingatia marekebisho yaliyofanyika kwenye sheria na kujikita katika masuala ya ununuzi na hilo litakuwa ni sharti la lazima.

“Lakini natoa wito kwa wataalamu kufanya uamuzi wa kizalendo ikiwa ni pamoja na kuwapa kazi Watanzania kwa kuwa nao wanauwezo sawa na makandarasi wa nje,” alisema.


Kwa upande mwingine alisema amepokea malalamiko ya maslahi madogo kwa wataalamu hao hasa kwa wahitimu cheti na kuahidi kuyatafutia ufumbuzi kwa sababu ni lazima wafanyakazi wote waheshimiane kwa kuwa ndio wanaosimamia bajeti kwa asilimia kubwa.

Alimuagiza mtendaji mkuu na katibu mkuu kuwasilisha malalamiko hayo ofisini kwake ili yafanyiwe kazi haraka.

Mwenyekiti wa Bodi ya PSPTB, Jacob Kibona, alisema bodi hiyo imefanikiwa kuhuisha mitaala ya mafunzo ya kitaaluma yenye kujikita katika umahiri ili kuzalisha wataalamu wenye ujuzi katika mnyororo wa ununuzi na ugavi.

Aalisema bodi hiyo imefanikiwa kuendesha kongamano la kitaaluma kila mwaka kwa lengo la kuwakutanisha wataalamu na wadau wa manunuzi na ugavi wa ndani na nje ya nchi ili kubadilishana uzoefu katika mnyororo wa ununuzi na ugavi.

Alisema bodi hiyo kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia ununuzi na ugavi imechangia kufanya mapitio ya sheria ya ununuzi kwa umma kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kupitia sheria kwa lengo la kuhakikisha inaleta tija zaidi katika ununuzi wa umma kwa kuzingatia bei halisi ya soko.





# Wodi, uzio vyajengwa kwa mil. 320/- Msalala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UJENZI wa wodi maalum ya wagonjwa wa dharura yenye vyumba vinane pamoja na msingi wa uzio katika kituo cha afya Bugarama, kilichopo Kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga vimetajwa kugharimu Sh. milioni 320 hali iliyomshtua Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga wakati wa ukaguzi wa kituo hicho.

Kati ya fedha hizo Sh. milioni 200 zilitumika kujenga boma la wodi hiyo huku Sh. milioni 120 zikitajwa kutumika katika ujenzi wa msingi wa uzio wa kituo hicho ambapo ujenzi huo unatekelezwa chini ya usimamizi wa Mgodi wa dhahabu wa Barrick Bulyanhulu.

Akitoa taarifa ya ujenzi huo juzi mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mdeme, Mratibu Idara ya Mahusiano wa Mgodi huo, William Chungu alisema, ujenzi wa wodi hiyo umetengewa dola za Kimarekani 95,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 200 hadi kukamilika kwake.

Alitaja msingi wa uzio unaozunguka kituo hicho kuwa umetumia Sh. milioni 120 na kufanya gharama zote kufikia Sh. milioni 320 huku wakiwa na mpango wa kuongeza majengo ili kituo kiwe hospitali kamili.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliingiwa na wasiwasi juu ya kiwango hicho kujenga wodi hiyo tena yenye vyumba nane tu kulinganisha kiwango hicho fedha cha Sh. milioni 200 kuwa kinaweza kujega zahanati mbili pamoja na vifaa tiba na kuanza kutoa huduma kwa wananchi na kuagiza vyombo vya dola kuchunguza gharama hizo.

Alisema, tathmini ya gharama za ujenzi wa wodi hiyo pamoja na msingi wa uzio unaozunguka kituo cha afya zipitiwe upya, kwa kuwa hakuridhishwa na gharama zilizotajwa kutumika na kwamba gaharama hizo bado zitaongezeka pia kwenye kununua vifaa tiba na madawa na kumwagiza Katibu Tawala wa mkoa kuunda timu ya uchunguzi.

"Ndugu zangu wananchi sisi serikali tunajenga zahanati zetu vijiji hadi kukamilika na kuwa na vifaa tiba na madawa kwa gharama ya Sh.milioni 100, kiasi kilichotajwa hapo cha Sh. milioni 200 ni zahanati mbili, wangesema zimetumia Sh. milioni 60 ningekubali, lakini hii hapana," alisema Mndeme.

Katibu Tawala mkoa, Profesa Siza Tumbo, aliahidi kutekeleza agizo hilo kwa kuunda kikosi kazi ambacho kitafika na kuanza kupitia upya gharama za ujenzi wa wodi hiyo na kuwataka wahusika kutoa ushirikiano watakapoanza kazi ya kupitia gharama hizo.

Awali, akitoa taarifa ya kituo hicho, Maganga Mkuu wa Halmashauri ya Msalala, Dk. Sisti Mosha alisema, kituo kinahudumia wakazi 48,000 na kata na vijijini jirani vya Mkoa wa Geita kama vile Bukoli, Shaende, Nyaseki, Nyakagwe na Iyenye na kwa wastani wanahudumia wagonjwa 836 kwa mwezi.

Alisema, wana mpango wa kukipadisha hadhi na kuwa hospitali kwa kujenga wodi ya watoto, upasuaji wanaume na wanawake, jengo la dharura, maabara kubwa, phamasi na jengo la magonjwa ya mlipuko na sasa jengo la mionzi limekamilika na wanatafuta wafanyakazi wawili ili waanze kutoa huduma kwa wananchi.



Mkuu wa mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akiwasha trekta alilokabidhiwa wakati wa hafla ya mgodi huo kukabidhi vituo viwili vya raslimali kilimo (Agricultural Resources Centres) vya Mwendakulima na Mondo kwa Serikali iliyofanyika wilayani Kahama Jana.Wengine pichani ni Wafanyakazi wa Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wasaidiwa mbinu kilimo bora

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, amewataka Maofisa Ugani ngazi zote wilayani humo kuwasaidia wakulima kupata mbinu za kuwawezesha kufanya kilimo bora katika kipindi cha mvua ya mfululizo ili kukabiliana uharibifu wa mazao unaotokana na mvua hizo.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ugawaji wa pembejeo za kilimo kwa wananchi wa Kijiji cha Ngunga, wilayani humo, ambao wamepitiwa na mradi wa umeme jua na kupisha maeneo hayo.

Alisema ni wakati wa maofisa hao kuwafikia moja kwa moja wakulima katika mashamba yao na kuwapatia elimu ya kilimo cha kisasa kwa vitendo ili wafanye kilimo chenye tija na kupata mavuno mengi.

"Msimu wa mwaka huu, kumekuwa na mvua nyingi, hivyo wakulima watembelewe na kupewa mbinu mbalimbali zitakazowasaidia kukabiliana nazo ili kudhibiti uharibifu na kuwasaidia kuwa na mavuno ya kutosha," alisema Mkude.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Dk. Sabinus Chaula, awali akitoa taarifa alisema hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa umeme jua, kwa urejeshaji wa hali za wananchi kiuchumi pamoja na kuwa na chakula ambao wamepitiwa na mradi huo.

"Pembejeo za kilimo ambazo wanapatiwa wakulima ni mbolea za kupandia na kukuzia mazao, viuatilifu, mbegu za choroko, alizeti, mtama na vifaa vya kilimo ambavyo ni majembe, panga, visu, pampu za kupulizia wadudu na vifaa kinga mabuti, mipira ya mikono na magwanda," alisema Dk. Chaula.

Aidha, alitaja idadi ya kaya zitakazonufaika na mradi huo kuwa ni 75 zenye wananchi 556, ambao watalimiwa pia na mashamba yao jumla ya Hekali 516, na watapewa na elimu ya mbinu bora za kilimo, ufugaji na utunzaji wa mazingira.

# Vijana 25,000 kunufaika mradi wa kilimo biashara

**Na Halima Ikunji,** TABORA

VIJANA zaidi ya 25,000 kutoka katika mikoa ya Tabora na Shinyanga wanatarajiwa kunufaika na Mradi wa Kilimo Biashara (VKB), unaotekelezwa na Shirika la Small Enterprises Institutional Development (SEIDA), kwa kushirikiana na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), utakaosaidia kuinua uchumi wa vijana hao.

Mradi huo ulitambulishwa hivi karibuni na Meneja wa Mradi, Frank Godlight Lyimo, katika warsha ya siku moja iliyofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora na kuhudhuriwa na Maofisa Maendeleo ya Jamii pamoja na kilimo kutoka wilaya za Igunga, Uyui, Nzega na Sikonge.

Godlight alisema mradi huo wa kimkakati unatarajiwa kutekelezwa katika halmashauri nane za mikoa hiyo miwili ambazo ni Igunga, Nzega, Uyui, Sikonge na Tabora na kwa Shinyanga ni Kishapu, Msalala, Ushetu na Shinyanga Vijijini. Alibainisha kundi litakalonufaika na mradi huo kuwa ni vijana wa kike na kiume walio na umri kati ya miaka 18-35 na asilimia 70 ya wanufaika hao ni wanawake na asilimia 70 ni vijana.

Godlight alifafanua kuwa kwa Mkoa wa Tabora jumla ya vijana 15,000 watahusika katika mradi huo na 10, 000 kwa Mkoa wa Shinyanga na mradi huo ni wa miaka mitatu ambao utekelezaji wake umeanza Oktoba 2023 hadi Septemba 2026 na mazao makuu yatakayolimwa ni alizeti, mtama na mboga.

Alisema wanufaika katika mradi huo watawezeshwa kuongeza kipato na kufanya uzalishaji wenye kukidhi mahitaji ya soko, kuhamasisha matumizi ya mbegu bora, kupunguza upotevu wa mazao wakati na baada ya mavuno na kufikia makundi ya watu wenye mahitaji maalum.

"Lengo kuu la mradi huu ni kuongeza kipato cha wakulima wadogo hususani vijana wa kiume na wa kike ikiwa ni sehemu ya kuboresha maisha na kuondokana na utegemezi katika kuajiliwa ili vipato vya kaya na jamii kwa ujumla," alisema Godlight.

Ofisa Kilimo wa mkoa huo, Modest Kaijage, alipongeza jitihada za uanzishwaji wa mradi huo na kuzitaja kuwa sehemu ya kuboresha maisha ya vijana katika mikoa husika.

Aliwataka vijana wa kiume na kike kuchangamkia mradi huo na ajira zitakazotolewa ili kujikwamua kiuchumi na kupitia mradi huo uzalishaji wa mtama na mafuta ya alizeti utaongezeka kwa wingi katika mkoa huo na kuinua uchumi wa wananchi wote.




Ukurasa 14

Kampuni yajitosa kuungana na serikali, wajibu wa kuhudumia wenye ulemavu




Tusipoangalia Historia ya Uhuru itapotea

Ukurasa 13



MSEMAJI SERIKALI VS TAMWA WALIPOKAA MEZA MOJA …

# Darasa la R4, falsafa anayoitumia Samia kuisuka nchi kimaendeleo

**Na Beatrice Moses**

R4, ni mkakati wa kifalsafa anayotumia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, akitaja inabeba dhana: Upatanishi au Maridhiano, (Reconciliation); Mageuzi au Mabadiliko (Reform), Ustahimilivu (Resilience) na Ujenzi Mpya (Rebuilding).

Anasema, kwa falsafa hiyo kueleweka vyema, vyombo vya habari vina nafasi ya kuwasaidia wadau, ikaeleweke, nchi isonge kimaendeleo.

Alisema hayo katika wasilisho lake kwenye Maadhimisho ya Miaka 36 ya Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake nchini(TAMWA), yaliyochukua siku mbili, mjini Dar es Salaam, kuanzia Novemba 28.

"Mfano hapo awali kulikuwa na zuio kwa vyama vya upinzani kufanya mikutano, serikali chini ya Rais Samia imeruhusu, pia kuna Tume ya Haki Jinai imefanya kazi kubwa wananchi wanapaswa kujulishwa," anafafanua.

Matinyi anaeleza, 'falsafa' ni dhana iliyozoeleka kwa wasomi vyuo vikuu, lakini inaweza kutumiwa kwenye hali ya kawaida, ikawa mwongozo mzuri kufanikisha mambo.

"Viongozi wana vitu vingi, wana sera, itikadi na falsafa. Siyo kila kiongozi kutangaza falsafa yake, wapo ambao hufanya utekelezaji wa kile anachokiamini kimya kimya," anasema Matinyi.

Anatoa mfano katika miaka ya 1960 hadi 1970, viongozi wengi waliendeshwa na itikadi, akimtaja Hayati Julius Nyerere, alivyoongozwa na 'Ujamaa na Kujitegemea.'



Naibu Waziri wa Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Injinia Kundo Mathew, alipotembelea mabanda ya maonyesho katika Maadhimisho ya Miaka 36 ya TAMWA, wiki tatu zilizopita. **PICHA: BEATRICE MOSES.**

Mantinyi, ambaye pia ni mwanahabari, anaeleza Rais Nyerere, aliwahi kuandika maoni mwaka 1970 kwenye gazeti la Tanganyika Standard, akivitaka vyombo vya habari kuibua maovu yanayotendwa na viongozi wasiotakia mema nchi.

**MARIDHIANO**

Matinyi anaifafanua kwa hiyo, akitumia simulizi ya kuwapo migogoro kadhaa ya kijamii, ikiwamo ya wakulima na wafugaji inayochukua miaka mingi na viongozi wa maeneo huyatatua.

Mfano mwingine anatumia ni msuguano kijamii, mathalan kati ya wajasiriamali maarufu 'Machinga' na serikali za mitaa. Sura inayotawala, wenyeviti wa maeneo wanatamka kusimamia sheria, machinga wanasimamia kutafuta riziki; pia ipo baina ya waendesha bodaboda na askari usalama barabarani.

"Bodaboda anapovuka taa bila kujali kama ameruhusiwa imefika, wakati askari anamtazama tu! Pia kwenye siasa vijana wa upinzani na chama tawala, kunaweza kuwa na migogoro ya makundi tofauti. Lakini ni vyema, kuwa na tabia ya kutafuta maridhiano, maana migogoro haijengi inabomoa," anasema.

Matinyi anaeleza kuwapo wananchi wenye tabia ya kuweka utani kwenye mambo yenye ukweli, akitoa mfano vifo katika baadhi ya maeneo (anayataja), pia kuanzishwa msemo 'kuchomoa betri' kuwa utani wenye maana 'kusahau mabaya yaliyotokea.'

Matinyi pia anazungumia purukushani kati ya wawekezaji na wananchi kwenye maeneo kadhaa, ikiwamo machimbo ya mgodi wa Nyamongo mkoani Mara, wananchi walipojikusanya kuvamia kiwanda hicho wakidai wanaporwa haki yao.

**USTAHIMILIVU**

Matinyi anayesimamia kwenye wasilisho hilo kuwa mwalimu wa nadharia R4, anasema kuna wanaokosa ustahimilivu wa kujiondoa kwenye matatizo, akitumia mfano binafsi, wakati anasoma:

"Kuna siku mwalimu aliingia darasani na kuanza kutandika wanafunzi bakora. Wapo walioweza kuvumilia hawakujigusa walipotandikwa. Mimi na rafiki yangu tukatazamana na kuruka dirishani, kwa sababu tulikosa uvumilivu."

Anaeleza, Watanzania wameshavumilia mengi, kiasi kwamba nchi ikapata pongezi mwaka 1978, baada ya vita kumkabili Nduli Idd Amin Dada. Mwalimu Nyerere, wakati huo Rais wa kwanza nchini, akatangaza miezi 18 ya kujifunga mkanda, baadaye ukageuka utani 'imekuwa miaka 18.'

"Kwa kawaida watanzania wana ustahimilivu. Mfano janga la Uviko 19, kiongozi wa wakati huo aliweka msimamo ambao hakutaka watu kujifungia ndani, hatua ambayo ilisaidia nchi isiyumbe kiuchumi wakati nchi nyingine zikishuka. Tanzania haikushuka chini ya 'nne' na baada ya muda mfupi ilifikia tano," anasema.

**MABADILIKO**

Anataja mabadiliko ni yenye maslahi kwa nchi, akirejea Rais Dk. Samia baada ya kuanza kuongoza nchi, kulikuwapo pumziko kubwa lililotolewa na mtangulizi wake, kuzuia mikutano ya kisiasa, lakini yeye akaruhusu.

Pia, anasema Dk. Samia, akaanzisha Tume ya Rais ya Kushughulikia Haki Jinai, iliyoongozwa na mwanahabari, Dk. Ayub Rioba, akieleza imefanikiwa sana.

Anataja mifano, mabadiliko yamefayika kwenye sekta za elimu, kamati iliyoongozwa na Jackson Makweta kutumia Kiswahili kwenye ngazi zote.

Pia, sekta ya afya, dawa zote za msingi sasa zinapatikana kuanzia kwenye zahanati hadi hospitali kubwa, zikisimamiwa na Bohari ya Dawa (MSD) na sasa rasmi, Bima ya Afya ni kwa wote.

**UJENZI MPYA**

Matinyi anatumia kigezo cha filamu Royal Tour, ilivyosaidia kuongeza idadi ya watalii nchini, akatumia mfano Hifadhi ya Ngorongoro, sasa kila siku inapokea watalii 150.

Pia, anaitaja miundombinu nchini kuendelea kuboreshwa, kufufuliwa Shirika la Ndege Tanzania (ATC), Shirika la Reli Tanzania (TRC), pia barabara kitaifa na ushirikiano katika Muungano, teknolojia iliyofanyiwa majaribo Zanzibar, imethibitika kuwa nzuri, itahamishiwa Tanzania Bara, kujenga barabara imara za changarawe.

UCHUMI

## ZAO LA MIAKA 62 YA UHURU

# Chuo cha Ustawi wa Jamii; mtaji wa maendeleo uliolima shamba la Nyerere, leo unapalilia kwa Samia

**Na Dk. Dominic Nkolimwa**

CHUO cha Ustawi wa Jamii ni miongoni mwa vyuo vya elimu ya juu nchini vinavyomilikiwa na serikali, ambapo Desemba hii kinatimiza miaka hamsini tangu kuanzishwa kwake mwaka 1973.

Wakati kinaanzishwa ni miongoni mwa maudhui ya Mpango wa Maendeleo wa Pili nchini, 1969 hadi 1974, kuisaka nchi kiimaendeleo.

Jukwaa likawa, l ikijielekeza kuendelea kuandaa watalaam, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii ya kitanzania, Afrika na Dunia.

Chuo hicho kinachotimiza nusu karne, kilianzia katika majengo ya kukodi ya Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) Kurasini, kabla ya kuhamia eneo la Kijitonyama, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam mwaka 1975.

Chuo hicho kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mwaka 1973 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2002, ni miongoni mwa Taasisi za elimu ya juu zilizoanzishwa miaka 12 tu baada ya uhuru wa iliyokuwa Tanganyika (sasa Tanzania) kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo katika jamii.



Wahitimu katika Mahafali ya 47 ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, chuoni Kijitonyama, siku chache zilizopita, Dar Es Salaam. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Kuanzishwa kwake, kulilenga kuandaa wataalamu katika fani ya ustawi wa jamii, maendeleo ya jamii na fani zinazoshabiana nazo, kama inavyoaanishwa katika mipango na miongozo kila mara serikalini. Chuo pia kimetumiwa na nchi mbalimbali za Kusini mwa Jangwa la Sahara, zikiwamo Msumbiji, Angola, Zimbambwe, Afrika ya Kusini, Namibia, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Zambia, Malawi, hata Sudan, katika kuandaa watalaamu wa fani ya ustawi wa jamii.

Leo hii, kinapoadhimisha miaka 50, kimewajengea historia kubwa watu wengi waliopita hapo, sasa wametawanyika sehemu mbalimbali, ikiwamo, Asia, Afrika, Amerika na hata Ulaya wakihudumu katika shughuli mbalimbali za kiserikali na binafsi ili kuistawisha jamiii katika mataifa yao.

Chuo pia katika majukumu, ilikuwa ni kimbilio kwa wananchi, ambao nchi zao zilikuwa katika mapambano ya kudai uhuru katika kuandaaa wataalamu, wakati mataifa hayo yakipambania uhuru na ikizingatiwa mchango mkubwa wa Tanzania katika juhudi za kusaidia nchi hizo ili ziweze kujitawala.


> “
> **Leo hii, kinapoadhimisha miaka 50, kimewajengea historia kubwa watu wengi waliopita hapo, sasa wametawanyika sehemu mbalimbali, ikiwamo, Asia, Afrika, Amerika na hata Ulaya wakihudumu katika shughuli mbalimbali...**

Chuo cha Ustawi wa Jamii, sasa kiko katika historia ya kupitia hatua mbalimbali za maendeleo hadi kuadhimisha miaka 50, ukizingatia ukweli kwamba shughuli za Chuo cha Elimu ya Juu, kama Usatawi wa Jamii ni kutoa huduma za kielimu zinazoambatana na mahitaji mengi ya rasilimali fedha na watu, ili kuboresha upatikanaji huduma bora ya kujifunza na kujifunzia.

**MAJUKUMU MAKUU**

Kazi kuu ya kwanza ya chuo, inatajwa hiki ni kuandaa wataalamu katika nyanja mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii, kwa maendeleo mapana ya mtu mmoja mmoja, jamii na taifa kwa ujumla.

Pili, inatajwa jukumu la kufanya tafiti zinazoibua changamoto zinazoikabili jamii na kuzitafutia ufumbuzi wa kitalaamu, ili kuwa na jamii inayojitambua na yenye kutambua umuhimu wa maendeleo ya kisayansi, kiuchumi, kisiasa na hata kijamii.



Mwenyekiti wa Bodi ya Magavana wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii Mhe. Sophia Simba akizungumza wakati wa Mahafali ya 47 ya Taasisi hiyo Desemba 08, 2023, Dar Es Salaam.

Kazi kuu ya tatu, inaangukia katika kutoa ushauri wa kitalaamu, baada ya kufanyika kwa utafiti, kuna mambo yanayoonekana kuwa changamoto katika jamii na kushauri njia iliyo bora katika kuondokana na changamoto hizo.

Chuo katika kuimalisha shughuli za kitafiti chuo hapo, kimekuwa kikitenga fedha kila mwaka ili kuimarisha shughuli za kitafiti, ambapo wahadhari waandamizi wamekuwa wakishirikishwa wahadhiri wachanga katika tafiti hizo ili kuwajengea uwezo katika tafiti.

Mathalani katika miaka ya hivi karibuni, chuo kimefuatiliaa athari za ajira za utotoni na chanzo chake, ambao ulionyesha chanzo kikubwa cha ajira hizo ni umasikini na athari zake kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Utafiti mwingine ulikuwa ni mchango wa mitandao ya kijamii katika kuchochea mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini.

Ikabainika kuwa vijana wengine wamekuwa wakitumia vibaya maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa kuelekeza akili zao zote katika mambo ya hovyo baadala ya mitandao hiyo, kuwasaidia kujipatia maarifa chanya kwa maendeleo yao binafisi na Taifa kwa ujumla.

Aidha, baadhi ya kazi za ushauri elekezi zilizofanywa na na chuo ni pamoja na; Mradi wa

Ulinzi na Usalama wa Watoto (Child protection) unaofadhiliwa na UNICEF; Usimamizi wa

Ujenzi kuna eneo la miundombinu ya kijamii kwenye Mbuga za Wanyama; Tathmini ya Athari za kijamii zitokanazo na Ujenzi wa Bomba la Mafuta (EACOP), kuwajengea uwezo Walezi kuhusu Malezi na Makuzi ya Watoto chini ufadhili wa Shirika la SoS Children Villages, pamoja na Tathmini ya Program Jumuishi ya Kitaifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM).

**MIRADI YA UBIA**

Pia, Chuo Cha Ustawi wa Jamii, kimeendeleza ushirikiano na taasisi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Mathalani, chuo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Agder- Norway, inatekeleza mradi wa NORHED wa miaka sita, kuanzia 2020 hadi 2026.

Ni mradi huu unaojikita katika maeneo matatu ya ushirikiano, ambayo ni kusomesha watumishi kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, kutoa fursa ya wanafunzi wanaotoka katika kaya masikini kujiendeleza kimasomo katika ngazi ya shahada ya uzamili.

Hadi sasa wanafunzi 10 wamefaidika na mradi huo. Aidha, unatajwa mradi umeanzisha programu ya Maabara ya Jamii katika mikoa mitatu (3) ambayo ni; Tanga, Mtwara na Iringa. Programu hizi zinalenga katika kuwajengea uwezo wananchi kuona fursa za maendeleo zilizopo katika maeneo yao na namna ambayo zinaweza kutumika kuwaletea maendeleo.

Kupitia programu hiyo, wanafunzi hutumia muda a miezi mitatu (3) wakiishi na kufanya kazi katika jamii husika.

Chuo pia kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi cha Klugenfurt - Austria, inatekeleza mradi wa ushirikiano wa PRO-WOMEN/ Africa-UniNet. Mradi huu una maeneo mawili ya kushirikiana; eneo la kwanza ni kufadhili utafiti katika eneo la mifumo ya kijamii inayosaidia kupunguza vitendo vya ukatili katika jamii kwa mikoa ya Tanga, Mbeya na Mara.

Eneo la pili ni kuwezesha wanafunzi na wahadhiri kutembelea nchi za Austria na Tanzania kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoezi katika mafunzo na taaluma ya Ustawi wa Jamii. Mwaka 2022.

Chuo kilipeleka wanafunzi wanne na walimu wawili (2) nchini Austria kuhudhuria mafunzokwa vitendo kwa kipindi cha miezi mitatu. Vilevile mhadhiri mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Klugenfurt-Austria alitembelea taasisi kwa ajili ya kubadilishana uzoefu na kujifunza, pia katika taaluma ya Ustawi wa Jamii.

Chuo pia kina jarida la kitaaluma linalochapishwa katika nakala ngumu na nakala laini ambalo hutoka kila mwaka mara moja na wakati mwingine mara mbili.

Jarida hilo linalenga kuchochea, na kuendeleza wanataaluma katika maandiko ya kitaluma, kutokana na tafiti mbalimbali zinazofanywa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na hata kisayansi.


Jarida hilo linalojulikana kama Jarida la Ustawi wa jamii ni miongoni mwa mafanikio lukuki sasa.

- **Mwandishi wa makala hii, ni Mhadhiri katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, na alishawahi kuwa mwandishi wa gazeti Nipashe.**

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tusipoangalia Historia ya Uhuru itapotea




MIONGONI mwa masomo muhimu yanayofundishwa shuleni kuanzia msingi, sekondari hadi vyuoni ni la Historia, ambapo lengo ni kufundisha

jamii ilikotoka, ilipo na hata inakokwenda.

Somo hilo mbali ya kufundishwa kama somo linalojitegemea, hata katika dini hufundishwa ili kujua waasisi wa dini, ni kina nani walitoka wapi na

walitokea tokea vipi.

Hivyo wafuasi wa dini katika kujifunza dini zao, hufundishwa watakatifu wao wakiwamo Yesu au Issa bin Mariam na hata mitume wengine walikotoka na walifanya nini.

Ndiyo sababu hata leo kisiasa jamii inakuwa na sherehe mbalimbali za kihistoria, huku upande wa dini hilo pia likifanyika kwa kuwa na sherehe za kuzaliwa watakatifu na mitume.

Mataifa mbalimbali yamekuwa yakiadhimisha siku za uhuru kukumbuka jinsi yalivyoondokana na utawala wa kimabavu, utawala uliokuwa wa minyororo na hivyo kuikata na kupata uhuru.

Lakini pia kuna nyakati mataifa hayo huadhimisha ushindi katika mambo mbalimbali yakiwamo ya vita kati ya Taifa moja na lingine na hivyo

kupata fursa ya kujijenga kama mataifa huru.

Bado zipo sherehe za kidini kama vile Pasaka, Krismasi au Noeli, Iddi el Fitri na Idd el Hajj lakini pia Maulid nakadhalika, zote hizo zikiwa ni kumbukizi za matukio mbalimbali ya kihistoria, sisi Watanzania tuna siku kuu kubwa kila Desemba 9, ambapo awali wananchi walikuwa wakihudhuria katika viwanja na kushuhudia matukio mbalimbali zikiwamo gwaride na ngoma, hata kwaya na kumaliziwa na hotuba.

Hiyo ni siku ya kukumbuka kushushwa bendera ya Mkoloni na kupandishwa bendera ya taifa huru la Tanganyika, katika sherehe zilizofanyika usiku wa manane katika uwanja wa Taifa, ambako leo ni wa Uhuru, Dar es Salaam.

Kwa Zanzibar, ambayo ilikuja kuungana na Tanganyika Aprili 26, 1964, baada ya kujipatia uhuru wake kutoka kwa Sultani, nayo imekuwa ikiadhimisha Mapinduzi yake ambayo ndio Uhuru wenyewe kila Januari 12, 1964.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

Miaka yote ya nyuma kabla ya awamu ya tano ya uongozi wa nchi hii chini ya Dk. John Magufuli, Watanzania ilipokuwa inafika Desemba 9 kila

mwaka, walikuwa wakiadhimisha kwa nguvu zote siku ya Uhuru wa Tanganyika.

Ndiyo maandalizi ya siku hiyo yalifanyika maeneo mbalimbali, yakiambatana na matumizi ya fedha, kutokana na uzito na heshima ya siku hiyo, lakini Rais Magufuli, alikataa akisema hapana tusifanye mashere-he tunachoma fedha bure.

Akaelekeza fedha zikajenge barabara ya Moroco-Mwenge, miaka mingine ikawa hivyo hivyo ya sherehe kimya kimya, kuchelea kuteketeza fedha ambazo ni kweli kuna mahali watu walikuwa wakijinufaisha.

Fedha zikapelekwa kujenga hospitali Dodoma ikaitwa Uhuru na ipo pale barabarani tu inawaka kiroho mbaya, watu wanatibiwa pale kuliko fedha hizo, zingeishia mikononi mwa wajanja wanaojifanya kumsaidia Rais, kumbe ni watafunaji. Mwanza nako wakafaidika kwa kujengewa barabara kutoka uwanja wa ndege kwenda mjini. Watu wakanufaika kwa miundombinu, ili fedha hizo zisiishie kwa mafisadi.

Awamu iliyofuata pia ikafuata nyayo hizo hizo, kwamba ya nini magwaride na watu kutumia fedha za umma, bora ziende angalau mahali zikafanye kazi.

Bila shaka mwaka huu hapakuwa na jinsi, kwani siku yenyewe ilifika tukiwa kwenye maombolezo ya mafuriko ya maji na maporomoko ya udongo wa Mlima Hanang na kupoteza ndugu zetu karibu 90 na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kama kawaida yake ya kuwa na moyo wa ubinadamu, akaona ya nini kufanya magwaride na kula fedha wakati ndugu zetu wako msibani na wengine wakiuguza majeraha.

Akaagiza hizo za miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika ziende zikawashike mikono ndugu zetu, kwa kuwarejeshea miundombinu na makazi ya kudumu sambamba na vifaa na samani zao.

Watanzania tunamshukuru Rais Samia kwa kulifanya hilo na aendelee kulifanya, lakini tukumbushane kuwa Sikukuu ya Uhuru ni muhimu kwetu lakini hasa kwa vizazi vijavyo. Bila kufanya sherehe zinazotukumbusha tulikotoka, basi Historia haitakuwa na maana tena si tu kwetu hata kwa vizazi hivyo, kwa sababu

hatutawakumbuka waliotufikisha tulipo hivi sasa. Shamrashamra zirejeshwe. Mungu endelea kutubariki Watanzania.

UCHUMI

# Kampuni yajitosa kuungana na serikali, wajibu wa kuhudumia wenye ulemavu

## •Wawe na uwezo wa kazi, wawajibike....




Maandamano ya watu wenye ulemavu katika maadhimisho ya siku ya walemavu duniani ambayo huadhimishwa kila ifikapo Desemba 3 ya kila mwaka, katika matukio tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Frank Monyo**

DESEMBA 3 ya kila mwaka ni Siku ya Watu Wenye Ulemavu Duniani. Mwaka huu, maadhimisho yalikuwa na maudhui ya ushirikiano katika hatua ya kuokoa na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, (SDGs) kwa pamoja na watu wenye ulemavu.

Malengo ya Dunia kwa Watu wenye Ulemavu, ni sehemu ya malengo ya maendeleo endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa. Hayo ni kuhakikisha maendeleo yanafanyika kwa njia endelevu yanayojumuisha kila sehemu ya jamii, ikiwamo wenye ulemavu.

Ni malengo yamejumuishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), na hasa Lengo la 10 linalotamka: Kupunguza tofauti ya kijamii na linahusisha kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma katika maendeleo.

Ulemavu, ni hali inayowafanya watu kupungukiwa uwezo wa kutekeleza shughuli zao za kila siku, ukiwa kwa namna mbalimbali, kama vile kimwili, kiakili, usikivu, kuona, au kisaikolojia.

Serikali nyingi duniani zinatambua umuhimu wa kutoa haki sawa kwa watu wenye ulemavu na kujitahidi kujenga jamii inayojumuisha kwa kutoa fursa sawa kwa wote, bila kujali hali zao za kiafya. Hiyo inajumuisha kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya, elimu, ajira, na miundombinu inayofaa kwa wenye ulemavu.

Katika jamii nyingi kuna harakati za kuboresha ufahamu kuhusu ulemavu na kuwasaidia wenye ulemavu kupata haki zao, wakashiriki kikamilifu katika jamii na kupata haki sawa ya ushirikishwaji.

Pia, teknolojia inaendelea kuchangia kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu, kwa kutoa suluhisho za kiteknolojia, zinazowawezesha shughuli zao za kila siku.

**SERENGETI YAINGILIA KATI**

Mkurugenzi wa Uhusiano wa Kampuni ya Serengeti Breweries, John Wanyancha, anasema kampuni imechukua msimamo kulingana na takwimu zinazohusiana na hali hiyo nchini.

Anasema nchini kunakabiliwa na uhaba kutokuwa na elimu juu ya watu kwa wenye ulemavu, kufikia asilimia 48 kwa idadi ya wenye ulemavu, ikilinganishwa na asilimia 25 kwa wasio na ulemavu.

Wanyancha anataja, kuna asilimia 3.1 tu ya wenye ulemavua wanaopata kipato kutokana na ajira ya kulipwa, akihimiza haja ya hilo kufanyiwa kazi kuleta mabadilioko yenye maendeleo.

"Tangu kuanzishwa kwa safari hii mwaka 2021, Serengeti Breweries Ltd imeungana na vyama vya PWDs (w3enye ulemavu) na kuajiri kwa mafanikio wafanyakazi wanne wa kudumu wenye ulemavu.

"Kampuni inalenga kuongeza idadi hii ifikapo 2026, ikitilia mkazo azma ya kuwa na mabadiliko halisi, ya muda mrefu," anasema Wanyancha. Anaongeza kuwa SBL inaendesha programu za mafunzo ya stadi za maisha kila mwaka, zinazowezesha mamia ya wenye ulemavu kupata maarifa muhimu ya ujasiriamali, kilimo na mipango ya biashara.

Wanyacha anasema, kampuni yao inachangia kuwawezesha na kuwajengea uwezo wa kujitegemea jamii hiyo akitumia mfano "mwaka 2021, kwa kushirikiana na Foundation of Disability Hope, Serengeti Breweries Ltd iliwasaidia zaidi ya PWDs 200 katika mafunzo ya kilimo biashara huko Dodoma."

Anaongeza: "Serengeti Breweries Ltd imejitokeza kama mwenezaji muhimu wa kujumuisha PWDs katika sekta binafsi ya Tanzania. Kupitia majukwaa mbalimbali, kampuni inahamasisha wadau, ikiwa ni pamoja na wale katika mlolongo wake wa usambazaji, kuiga mfano wake wa kuajiri PWDs, kutambua thamani kubwa wanayoileta kwenye nguvu kazi."

Eneo lingine analitaja katika msamiati: nguzo ya Moyo wa Maendeleo kwa Jamii ya Mwaka 2030, bali pia inachangia kwenye ajenda kubwa ya kitaifa ya kujenga jamii yenye kujumuisha zaidi na yenye usawa.

Anasema ni muhimu kwa jamii kutambua mchango na uwezo wa watu wenye ulemavu na kuhakikisha wanapata haki zao za msingi ili kujenga jamii endelevu na yenye usawa kwa wote.

Hapo kampuni hiyo inaeleza kuonekana uelewa kuongezeka kati ya kampuni za kibiashara kuhusu umuhimu wa kuwawezesha wenye ulemavu, huku wakitambua haja ya kuingilia kati hilo kwa kina nchini.

Utafiti unaonyesha kuwa, asilimia 13.2 ya kaya nchini zina mwanachama mwenye aina ya ulemavu, SBL ikilenga kuleta matokeo mazuri kwa kushughulikia changamoto zinazowakabili wenye uwezo tofauti.

Kwa kuzingatia juhudi za serikali ya Tanzania kukarabati pengo, programu ya wenye ulemavu ya Serengeti Breweries, inaakisi malengo katika Sera ya Kitaifa ya Ulemavu.

Serikali inasisitiza ushirikiano na wadau kuwawezesha PWDs, kuhakikisha wanapata zana za kazi na pesa za mbegu kwa miradi ya kujipatia kipato.

Wanyancha anasema, "Programu yetu ya PWDs imeundwa kimkakati kushughulikia changamoto tatu muhimu zinazokabiliwa na PWDs: ukosefu wa ajira, kukosa sauti ya pamoja ya utetezi, na haja ya ushirikiano.

Tumejiwekea lengo kubwa la kuwa na angalau 5% ya nguvu kazi ya kampuni ikiwa ni PWDs ifikapo 2026, ikionyesha azma yake ya kuwa kiongozi katika kujumuisha PWDs".





## HABARI DODOMA

# Mchengerwa awataka Ma-DED kuwa wabunifu kutatua kero za wananchi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amewagiza wakuu wa mikoa, makatibu tawala na wakuu wa wilaya kutoa ushauri kwenye halmashauri kuandaa bajeti zinazolenga kutatua kero za wananchi badala ya fedha nyingi kutumika kulipana posho. Mchengerwa alitoa agizo hilo jana kwenye hafla ya kukabidhi magari sita yaliyotolewa na serikali kwa halmashauri za mkoa wa Singida kwa ajili ya usimamizi wa sekta ya afya ili kuleta tija katika utoaji wa huduma.

Alisema kwenye maeneo mengi asilimia 60 na 70 ya bajeti inayopangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, nyingi imekuwa sehemu za posho na zingine zinatumika kinyume cha malengo hasa zile ambazo TAMISEMI inazipeleka kwenye halmashauri.

"Baadhi ya wilaya kumekuwa na changamoto ya uhaba wa madawati na uchakavu wa madarasa lakini katika hali ya kushangaza mkuu wa wilaya au mkurugenzi wa halmashauri anashindwa kuwa mbunifu na kusema hana bajeti na kusubiri hadi Rais apeleke fedha. "Kama mkurugenzi huwezi kununua hata madawati 100, kukarabati darasa moja, hutaki kuwa mbunifu na unasubiri hadi bajeti, nitakuweka pembeni utasubiri ukiwa nje ya mfumo na tutateua mwingine atakayekuwa mbunifu," alisema.

Mchengerwa alisema kwa kiongozi wa kuteuliwa ni vyema akajipanga na kuwa mbunifu kwenye maeneo yake kwa kuwa ziko kero ndogo ambazo zinaweza kumalizwa na wao wenyewe badala ya kusubiri hadi Rais, waziri au mkuu wa mkoa aseme.

Aidha, aliwagiza wakuu wa wilaya kushusha maelekezo chini kwa maofisa tarafa, watendaji wa kata na vijiji na wenyeviti wa vijiji wawe wanafanya mikutano kuzungumza na wananchi na wawe wanakagua muhtasari kuangalia kama kweli mikutano imefanyika.

Kuhusu magari hayo, alisema serikali inategemea kuona waganga wakuu wa mikoa na wilaya wanafanya vikao vya mara kwa mara vya watumishi kusikiliza kero zao na kuzipatiwa ufumbuzi na kukagua zahanati na vituo vya afya katika maeneo yao.

"Mkuu wa mkoa unapokwenda kwenye ziara wilayani ni vyema ukapata taarifa kama mganga mkuu wa wilaya amefanya vikao na watumishi lini na taarifa mtuletee. Tukibaini mganga mkuu wa wilaya hajafanga vikao tutamshughulikia kwa kumwondoa na kuweka mwingine kwani wako Watanzania wengi wanaotamani nafasi zetu tulizopewa," alisema .

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema katika kipindi kifupi mkoa umepokea magari 15 yakiwamo ya kubebea wagonjwa.



Naibu Katibu Mkuu Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu, Sayansi, Teknolojia, Habari na Ufundi stadi (RAAWU) Taifa ,Simon Mbai akizungumza wakati wa kufungua mafunzo kwa viongozi wa Kamati za Wanawake wa chama hicho Taifa yaliyofanyika Jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi wanawake wawakumbuka waathirika wa mafuriko Katesh

**Na Gloria Maganza,** DODOMA

MTANDAO wa Polisi Wanawake Tanzania (TPF NET), umetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa waathirika wa maafa ya maporomoko ya matope yaliyotokea Wilaya ya Hanang mkoani Manyara.

Msaada huo wenye thamani ya Sh. milioni 17.7 ulikabidhiwa jana jijini hapa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Dk. Jim Yonazi, na Kamishna wa Kamisheni ya Ushirikishwaji wa Jamii, Faustine Shilogile, na Kamishna wa Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Suzan Kaganda.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Dk. Yonazi alipongeza Jeshi la Polisi kwa jitihada mbalimbali walizozitoa ikiwamo kuwakumbuka waathirika wa maafa hayo na kwamba atahakikisha unawafikia walengwa.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Polisi Wanawake, Kamishna Kaganda, alisema mtandao huo uliona ni vyema utoe msaada kwa waathirika waliokutwa na maafa huko mkoani Manyara kwa ajili ya kuwafariji kutokana na kupoteza mali mbalimbali.

# Matukio unyanyasaji viongozi NGO wapungua

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAKAMU wa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Wakili Deus Nyabiri, amesema matukio ya unyanyasaji dhidi ya watendaji wa mashirika ya kiraia yamepungua kwa kiasi kikubwa kati ya mwaka 2021 hadi 2023.

Nyabiri aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua semina ya kuzijengea uwezo asasi za kiraia kuhusiana na masuala ya utawala bora iliyoandaliwa na TLS.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kwa asasi za kiraia kuelewa wanachokifanya ili kuelimisha umma kwa kuwa wao ni kiungo muhimu kati ya wananchi na serikali.

"Sasa tunakaribia kwenda kwenye uchaguzi je asasi zinajua mambo yanayohusiana na uchaguzi? zinajua sheria, kanuni za uchaguzi, mabadiliko yanayotokea," alisema Wakili Nyabiri.

Kwa mujibu wa Nyabiri, kuna haja kwa kila asasi kujua wajibu wake ili kuweza kutekeleza mipango na miradi yao kwa ufanisi kwa maslahi yao serikali na wananchi.

Alisema ni vyema kwa kila asasi za kiraia ikawa na ubobezi kwa kile wanachokitekeleza ili kuwe na ufanisi na kuleta mabadiliko kwenye jamii na taifa kwa ujumla.

Mtaalam wa masuala ya maendeleo sekta ya Asasi za Kiraia (AZAKI), Sia Ngowo, alisema utafiti wa msingi juu ya mazingira ya sera ya kisheria kwa ushirikishwaji wa AZAKI katika utawala wa kidemokrasia ulifanyika Tanzania Bara na Zanzibar (Mei na Juni 2023).

Alisema lengo la utafiti huo lilikuwa ni kukusanya taarifa za msingi kuhusu sheria, sera, na fursa za kiutendaji na changamoto za ushiriki wa AZAKI katika utawala wa kidemokrasia.

Alibainisha kuwa walibaini AZAKI zinakabiliwa na kero katika kutekeleza utetezi unaozingatia Ushahidi huku upatikanaji wa nyenzo muhimu kwenye nafasi ya kiraia ni mdogo kwa asilimia 46.

"Ripoti za kina za hali kuhusu wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu hazipo na asilimia 70 ya AZAKI zinakabiliwa na matatizo ya kifedha, jambo linalozuia uchangamfu na ushiriki wao,"alisema.





# Uzalishaji chakula hatarini kushuka

Na Nebart Msokwa, MBEYA

UZALISHAJI wa mazao ya chakula na biashara mkoani hapa kwa msimu ujao wa mavuno uko hatarini kushuka kutokana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kusambaza mbegu feki kwa wakulima.

Juzi maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI) walifanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye maduka yanayouza pembejeo za kilimo katika Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Mji wa Mbalizi na kubaini baadhi ya wafanyabiashara wakiuza mbegu feki.

Maofisa hao walichukua hatua mbalimbali dhidi ya wafanyabiashara hao, akiwemo mmoja wa Mbalizi kwa kumfungia duka lake na kumnyang'anya kibali cha kuuza mbegu nchini.

Ofisa Mfawidhi wa TOSCI Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Peter Nasari, alisema mfanyabiashara huyo, wamempiga marufuku kujihusisha na biashara hiyo ya kuuza mbegu nchini na kwamba wanatarajia kumfikisha mahakamani na wengine watakaobainika kukiuka sheria ya udhibiti ubora wa mbegu ili kukomesha tabia hiyo. "Tunatoa onyo kwa wafanyabiashara wengine wa mbegu kuhakikisha wanaheshimu sheria, sisi tunayo mamlaka ya kisheria kumnyang'anya mfanyabiashara yeyote kibali cha kuuza mbegu na kumfikisha mahakamani," alisema Nasari.

Aliyataja madhara ya kuwauzia wakulima mbegu feki kuwa ni pamoja na kutoota wakipanda mashambani na uzaaji hafifu, kuwasababishia wakulima hasara na kuhatarisha usalama wa hali ya chakula nchini.

Mkaguzi wa Mbegu TOSCI, Meshack Muhesi aliwataka wakulima kununua mbegu zenye nembo ya ubora inayotolewa na taasisi hiyo ili kuepuka kuuziwa mbegu feki na kupata hasara.

Aliwataka wakulima kuhakikisha wanapatiwa stakabdhi za kielektroniki baada ya kununua mbegu kama kielelezo zikileta shida.

Alisema wakaguzi wa TOSCI wapo kwenye halmashauri zote nchini kwa ajili ya kuwasiliana na wakulima ili kubaini wanaokumbana na tatizo lolote kuhusiana na mbegu kwa lengo la kuwasaidia.

" Wakulima wanapokumbana na tatizo la mbegu wanaweza kuwasiliana na mabwana shamba kwenye maeneo yao ambao watawasaidia kuwasiliana na wakaguzi wetu na taarifa zitatufikia, " alisema Muhesi.

Baadhi ya wafanyabiashara hao, walisema ukaguzi unaofanywa mara kwa mara na maofisa wa TOSCI kwenye maduka na maghala unasaidia kudhibiti wafanyabiashara wadanganyifu na wakulima kupata mbegu bora.

Grace Kessy, alisema ukaguzi huo unasaidia kuwakumbusha wafanyabiashara taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kutunza ubora wa mbegu.

Vilevile, alisema wakaguzi hao wanawapatia elimu sahihi ya biashara ya mbegu, maendeleo ya kilimo na kuwakumbusha sheria za kusimamia ubora wa mbegu.

Msimu wa kilimo kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula nchini unaendelea huku kukiwa na changamoto ya kusambazwa kwa mbegu feki.



Msururu wa magari yaliyokwama katika eneo la Iyunga jijini Mbeya juzi baada ya madereva daladala kufunga Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) ili kushinikiza serikali kuwasikiliza baada ya kutokea ugomvi baina yao na waendesha pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) ambapo magari hayo yalikwama kwa zaidi ya saa mbili kabla ya madereva hao kuondolewa na polisi. **PICHA NA NEBART MSOKWA.**

## RC Homera aagiza mhandisi, wenzake kuswekwa rumande

Na Nebart Msokwa, BUSOKELO

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo kumshikilia Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, Ibrahim Harith na wenzake kwa tuhuma za kuchakachua vifaa vya ujenzi wa nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Kingili.

Mhandisi huyo pamoja na wenzake wanatuhumiwa kuchakachua ujenzi wa nyumba hiyo ambayo inatakiwa kukaliwa na familia mbili kwa kile kilichoelezwa hauendani na kiwango cha fedha zilizotolewa.

Homera alibaini kuwa wataalamu hao wametumia nondo zisizokidhi ubora huku makaro ya kuoshea vyombo jikoni yakiwa ni madogo ikilinganishwa na kiwango cha fedha zilizotumika.

Aliagiza TAKUKURU kuchunguza mradi huo kuanzia mwanzo mpaka mwisho ili kubaini mapungufu mengine na kuwachukulia hatua watakaobainika kuchakachua mradi huo.

"Kuanzia sasa wanatakiwa wawe chini ya ulinzi mpaka tutakapomaliza ziara yetu, watatakiwa kuhojiwa na atakayebainika anatakiwa kuchukuliwa hatua," alisema Homera.

Akitoa maelezo ya mradi huo, Mhandisi Harith alisema utagharimu Shilingi milioni 100.

Alisema kwenye ujenzi huo walitumia nondo zenye ukubwa wa milimita 12 ambazo kitaalamu zilikuwa sahihi na kwamba baadhi ya mabomba kupasuka chanzo ilikuwa ni nguvu kubwa ya maji wakati yalipofunguliwa.

Homera na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo wanaendelea na ziara kwenye wilaya zote kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

# CCM waibana TARURA ujenzi wa mifereji

Na Elizabeth John, WANGING'OMBE

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe imemuagiza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Wanging'ombe kuhakikisha wanawaharakisha makandarasi kujenga mifereji kwenye barabara mpya na zilizopo ili kuepuka athari za mvua zinazondelea kunyesha nchini.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu wa CCM Mkoa wa Njombe, Julius Peter wakati wa kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho katika Kata ya Igosi kunakojengwa barabara za Igodivaha-Ujindile yenye urefu wa kilomita 8.6 na barabara ya Kipengere-Ing'enyango-Ujindile urefu wa kilomita 3.6 zenye thamani ya zaidi ya milioni 500.

Alisema CCM kwenye Ilani yake kiliahidi kitasogeza huduma kwa wananchi ikiwemo kuboresha miundombinu ya barabara.

"Kwa hiyo ni vema tukaelekeza mitaro ikatengenezwa wakati mnaendelea kutengeneza barabara hasa kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha na sio kwa barabara hii pekee bali na maeneo mengine mnayojenga barabara ambako hakuna mitaro pia tengenezeni ili ziwe imara na zipitike muda wote," alisema Peter.

Peter alitoa rai kwa TARURA kuhakikisha wanasimamia kiasi cha pesa ambacho kimetengwa na makadirio ambayo yamewekwa na serikali ili kilingane na matumizi halisi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) Mkoa wa Njombe, Samwel Mgaya alitilia mkazo ujenzi wa mifereji katika barabara hizo ili kuepuka uharibifu.

"Nimefurahishwa na ujenzi wa barabara hii lakini kama walivyoshauri wenzangu waliopita kama kutakuwa na uwezekano muongeze ile mifereji ili mvua ikiwa inanyesha isilete shida ya maji kukata barabara, " alisema Mgaya.

Awali Meneja wa TARURA Wanging'ombe, Boniface Kasambo, alisema ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe Igodivaha-Ujindile kilomita 8.6 na Kipengere-Ing'enyango-Ujindile (3.6) unafanywa na mkandarasi wa Kampuni ya M/s Gwena General Enterprises Company Limited.

Kasambo alisema mkandarasi huyo alipangiwa kufanya kazi mbalimbali ikiwemo kujenga tuta la barabara, kuchimba mifereji, kumwaga maji na kushindilia na kazi zote zinaendelea na kufikia asilimia 65.

Mwisho.



# Malaria yaua watatu, kasi ya ugonjwa yatisha

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATU watatu Zanzibar wamefariki kutokana na ugonjwa wa malaria kwa mwezi wa Novemba hadi Desemba, mwaka huu, huku kukiwa na idadi kubwa ya wagonjwa wakiendelea kupatiwa matibabu katika hospitali visiwani humo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, akijibu swali aliloulizwa na Nipashe kuhusu kasi ya ugonjwa huo visiwani humo jana, wakati wa kikao baina yake na waandishi wa habari jana wizarani kwake Mnazi Mmoja, alisema kasi ya ugonjwa huo ni ya kutisha.

Alisema kasi hiyo imetokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na sekta ya afya imeathirika kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha.

"Mvua hizi zimesababisha mbu wengi kuzaliana ikiwamo wa malaria na kuongezeka kwa maradhi na sasa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna wagonjwa wengi wa Malaria hali inayosababisha wagonjwa kulazwa hadi chini katika wodi kwa kukosa vitanda kutokana na idadi kubwa," alisema.

Alisema pia wapo wagonjwa wa Malaria ambao wanaendelea kupatiwa matibabu katika wodi ya uangalizi maalum (ICU) katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na wapo wagonjwa ambao Malaria imepanda kichwani na kupata uchizi.

Alisema wagonjwa wengi waliohojiwa wanatoka maeneo mbalimbali ya visiwa hivyo mjini na vijijini na kuitaka jamii kuchukua tahadhari ddhidi ya ugonjwa huo kwa kuhakisha wasafisha mazingira yanayowazunguka ili kuondosha mazalia ya mbu.

"Kuhifadhi ni bora kuliko kutibu kwa sababu kutibu ni gharama ni kubwa hivyo wananchi kuwa na ushirikiano katika kuhifadhi mazingira na kuhakikisha hakuna viashiria vinavyosababisha mazali ya mbu tuhakikishe hakuna majitaka yanayotuama," alisema.

Aidha, alisema serikali inafanya jitihada za kudhibiti ugonjwa huo ikiwamo kupiga dawa ya Malaria katika nyumba zote, lakini jambo la kusikiitisha baadhi ya wananchi wanakataa dawa hizo na katika Mji Mkongwe nyumba 40 zimekataa kupigiwa dawa hiyo.

Alisema sababu nyingine na maambukizi ya malaria ni watu kusafiri kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara, sekta ya ujenzi pia nayo ni sababu ya kuwa na wagonjwa wengi kwa sababu Zanzibar sasa kuna miradi mingi ya ujenzi na wanaojenga katika miradi hiyo wengi wao hawalali sehemu salama ambayo mbu hawatoweza kuwashambulia.

Mazrui alisema malaria Zanzibar ipo licha ya kufanikiwa kutokomeza ugonjwa huo upo chini ya asilimia moja, lakini katika kipindi hiki cha mvua idadi ya wagonjwa imeongezeka na ripoti kamili itatolewa Januari 2024.

Akizungumzia uzinduzi wa programu ya kitaifa ya wahudumu wa afya wa kujitolea Zanzibar ikiwa ni mara ya kwanza kuadhimisha siku ya wahudumu wa afya wa kujitolea ambayo itafanyika kesho na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi atakuwa mgeni rasmi, alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, mashirika na taasisi mbalimbali wanaimarisha afya za Wazanzibari kupitia mpango wa kitaifa wa wahudumu wa afya wa ngazi ya jamii.

Alisema wizara yake inashuhudia mafanikio na maendeleo makubwa ya kiafya kwa wanajamii kupitia program hiyo hasa katika kufikia dhamira ya Shirika la Afya duniani ya upatikanaji wa afya kwa wote.

"Zanzibar ni nchi ya mwanzo kwa Afrika Mashariki na kwingineko duniani kusimamisha mpango wa kitaifa wa wahudumu wa Afya wa ngazi ya jamii wanaotumia mfumo wa kidijitali ambao wanafanya kazi kwa kutekeleza vipaumbele vya serikali na mipango ya nchi," alisema.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii "Twende pamoja kuwaunga mkono wahudumu wa afya ngazi ya jamii, kuelekea afya kwa wote". Yatafanyika katika viwanja vya Maisara Suleiman Mnazi Mmoja.



Wakili Dickson Matata (kushoto), akiwaelekeza jambo wanachama wa Chadema katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana kabla ya kuanza kusikilizwa kesi waliyoifungua ya kupinga Ubunge wa wabunge 18 wa chama hicho akiwemo Halima Mdee. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Uwekezaji mradi maabara za kisasa kupaisha ufaulu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UWEKEZAJI wa Mradi wa Maabara za Kisasa katika shule mbalimbali za Zanzibar utasaidia kuimarisha upatikanaji wa elimu visiwani humo na hakuna sababu ya wanafunzi kutosoma na kutofaulu masomo ya sayansi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Leila Muhamed Mussa, alisema hayo katika makabidhiano ya maabara 10 na vifaa vya kisasa, kupitia mradi wa kuimarisha elimu sekondari, unaofadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Korea (KOICA) chini ya usimamisi wa United Nations Office for Project Services (UNOPS), Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema Serikali ya Zanzibar itahakikisha inahudumia na kuzisimamia maabara zote kwa kuingiza vifaa vya kutosha vya Maabara (Laboratories) na kemikali zinazohitajika kupatikana kwa wakati.

Alisema, upatikanaji wa maabara hizo 10 utasaidia kuondoa changamoto za wanafunzi kushindwa kufanya mazoezi ya vitendo kwa masomo yote ya sayansi sekondari.

Aidha, alisema ujenzi wa maabara hizo ni utekelezaji wa maelengo ya maendeleo endelevu na mkakati ya wa serikali kuhakikisha mazingira bora na jumuishi ya upatikanaji wa elimu katika visiwa hivyo.

Waziri Leila, aliishukuru Serikali ya Korea (KOICA) na wasimamizi wa mradi huo, UNOPS kwa kuunga mkono jitihada za serikali kuimarisha sekta ya elimu visiwani na kusimamia vizuri hadi kukamilika kwa maabara 10 katika viwango vizuri na uwekaji wa vifaa vya masomo matatu ya sayansi ambayo ni Fizikia, Kemia na Baolijia.

Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja, Sadifa Juma Khamis, aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuwaozesha mapema watoto wao badala yake kuwaendeleza na masomo. Meneja msimamizi mradi wa kuimarisha elimu ya sekondari Zanzibar, kutoka UNOPS, John Bundu Fofanah, alisema wamefanikiwa kukamilisha mradi wa kusaidia shule za sekondari Zanzibar kwa kujenga maabara 10 za sayansi na kuweka vifaa kwa shule tano Unguja na tano Pemba.

Alisema mradi huo ulihusisha maeneo matatu, ikiwamo ujenzi wa dahalia za wanafunzi, maabara za kisasa na kuimarisha uwezo wa walimu kwa kuwapatia mafunzo walimu 300 wa Unguja na Pemba, na kugharimu dola milioni tatu.

Mkurugenzi wa KOICA nchini Tanzania, Manshik Shin, alisema Shirika lake linafuraha kuanzisha maabara hizo 10 za Sayansi katika shule 10 kwa lengo la kutoa elimu bora ya sayansi kwa wanafunzi wa sekondari na sayansi na teknolojia ni misingi imara utakaochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Zanzibar.

Alisema Serikali ya Korea kupitia KOICA kwa kiasi kikubwa, imeweka misingi ya urafiki na Serikali ya Zanzibar na kusaidia kuimarisha masula ya sayansi na teknelojia, maabara hizo zimegharimu Sh. bilioni 7.7.

# Ujenzi hospitali za wilaya wasaidia kupunguza vifo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Muuguzi kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Mwanaisha Juma Fakihi, amesema ujenzi wa hospitali za wilaya umesaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto baada ya wajawazito kupatiwa huduma bora.

Alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara ya Afya umuhimu wa kuwakinga wajawazito na watoto, yaliyofanyika Chuo cha Afya Bweni nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema maradhi yasiyo ambukiza ni tatizo kubwa kwa kinamama na watoto, lakini kwa sasa vifo vimepungua tofauti na kipindi cha nyuma, lakini bado jitihada zinahitajika katika kutoa elimu wakati wote wa ujauzito.

Alisema wameshatoa mafunzo kwa madaktari 75 jinsi ya kuwahudumia kinamama na watoto wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

"Elimu tuliyowapa sio tukuwashughulikia jinsi kujikinga na maradhi yasiyo ambukiza lakini pia kuwa na lugha nzuri wakati wanapo toa huduma kutoka katika vituo mbalimbali unguja na pemba," alisema.

Mwalimu wa shule ya afya kutoka chuo kikuu cha Zanzibar, Mansab Ramadhan Mansab, alisema mradi huo wa kujikinga na maradhi yasiyo ambukiza lengo ni kuona mama na mtoto anakuwa salama wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua.

Mkufunzi wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Kenya, Peter Nandi Kave, alisema Afrika ya Mashariki katika kipindi cha nyumba vifo vya mama na watoto vilikuwa vingi ndiyo maana ya kuandaliwa kwa mradi huo.

Alisema magonjwa ya malaria na vifua kikuu ilikuwa changamoto kubwa kwa nchi maskini hasa za Afrika ya Mashariki, lakini kwa sasa wazazi wengi wamepatiwa elimu na madaktari wamefanya wajibu wao.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wa shule hiyo, Nawaje Habibu, alisema kabla ya kumaliza maabara wanafunzi wao walishindwa kupata uzoefu mzuri na kupata changamoto.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JORDAN RENATUS SHAWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2074-0039 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MSINDO SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NTM/RB/946/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



KARIMU BURHAN MOHAMED anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2762-0155 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia HALISI SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/ILA/7693/2023.

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAKARANGA KAKULU CHARLES** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0709-0178** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BUKONGO SEKONDARI** mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/ROM/2203/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**MOHAMED OMARI MWALIZA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye usajili MC 530 CMS kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu naye. **TAARIFA YA POLISI: PHQ/PWA/KIB/4458/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**FREDRICK GERSON KISANFU**
anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 455 ASC yenye jina la umiliki la KAHAMA IMPORT & EXPORT COMMERCIAL AGENCY LTD. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/SHI/KAH/1464/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMAR ABDALLAH KHALFAN** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY yenye usajili T 175 DHR, kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu naye.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/TAN/3289/2023**

**FOMU MADAI - 3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA MTWARA**
**KITUO CHA MTWARA – MJINI MKOA MTWARA**
**SHAURI LA MADAI/NDOA NA. 29/2023**
**JINA LA MDAI OSMUNDA JOSEPH KAPINGA**
**NA**
**JINA LA MDAIWA SELVESTA ALI MLACHA**

**KUITWA SHAURINI**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**KWA: SELVESTA ALI MLACHA**
**KWA KUWA MDAI/WADAI AMELETA/WAMELETA MADAI YAKE/YAO KWAMBA**
**KUVUNJA NDOA NA MGAO WA MALI YA NDOA**
**KWA HIYO** unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 28 mwezi wa 12 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza usikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 07 mwezi wa 12 mwaka 2023.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......129/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: AZIZA RAJABU KIMBUNGA wa MAFISA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA MRISHO HAKIMU KING'OMELA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 12 mwaka 2023

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**






TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Israel yasisitiza haitaacha vita hata kama dunia itawatenga

**TEL AVIV, Israel**

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amesema jeshi la nchi yake litaendelea kufanya mashambulizi maeneo ya Ukanda wa Gaza hata kama mataifa ya nje hayaungi mkono.

Netanyahu alisema hayo kufuatia juzi Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kupiga kura ya kupitisha azimio la usitishwaji mapigano kati ya jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas.

Waziri Mkuu huyo alisisitiza kwamba hakutakuwa na mjadala wowote kuhusiana na suala hilo.

Kulingana na taarifa kutoka ofisi yake, Netanyahu, alisema hayo kwa njia ya radio wakati akizungumza na wanajeshi walioko katika mapambano Ukanda wa Gaza.

Mataifa mbalimbali yameendelea kutoa wito wa kusitisha mapigano kutokana na uhalifu wa hali ya juu wa kivita kwenye eneo hilo la Wapalestina.

Hivi karibuni Rais Joe Biden, ambaye ni mshirika mkubwa wa Israel alikaririwa akisema kwamba Israel imeanza kupoteza uungwaji mkono kutokana na mashambulizi hayo.

"Hivi vita vitakuwa ni vigumu. Lakini ninaona, na hata nyie mnaona kuanza kusambaratika kwa Hamas. Ninaona watu wanaanza kuelewa kwamba tumedhamiria kuendelea hadi mwisho na kulisambaratisha kundi hili." alisema Netanyahu.

Wakati huo huo, mshauri wa usalama wa Ikulu ya Marekani, Jake Sullivan anatarajiwa kufanya ziara Israel kwa ajili ya kukutana na Netanyahu.

Msemaji wake John Kirby, alisema Sullivan atafanya mazungumzo mazito na kuna matarajio kwamba yatakuwa yenye kujenga.

Sullivan pia anatarajiwa kukutana na Baraza la Mawaziri linaloshughulikia vita hiyo pamoja na Rais wa nchi hiyo Isack Herzog.

Sullivan alikutana na mwanamfalme wa Saudi Arabia Mohammed bin Salman juzi na kujadiliana mchakato wa kupatikana kwa amani ya kudumu kati ya Israel na Palestina.

Walizungumzia pia suala la usitishwaji wa mapigano ikiwa ni pamoja na namna ya kuongeza shehena ya misaada muhimu Gaza

Wakati hayo yakijiri, Israel jana ilifanya mashambulizi 250 katika maeneo mbalimbali ya Gaza kwa kutumia vikosi vya angani, majini na ardhini.

Mashambulizi hayo yalijibiwa na Hamas kwa kurusha maroketi kuelekea Israel kwa mara nyingine.

Hata hivyo, jeshi la Israel (IDF) lilisema lilifanikiwa kuyadungua na moja ya mabaki ya roketi liliangukia katikati ya soko katika mji wa pwani wa Ashdod.

Kutokana na eneo hilo kuwa la hatari, waandishi wa habari 17 wamefariki wakiwa kazini hadi kufikia mwezi Oktoba.

Shirika la habari la RSF lilisema idadi hiyi ya kushtusha inahusisha waandishi 13 waliofia Ukanda wa Gaza, mmoja Israel na watatu nchini Lebanon.

Kiongozi wa Hamas, Ismail Haniyeh, alionya mpango wowote utakaochukuliwa baada ya vita utakuwa wa udanganyifu kama hautashirikisha kundi la Hamas.

"Tuko tayari kujadili mawazo au mipango yoyote ambayo inaweza kukomesha uchokozi wa Israel na kufungua ukurasa mpya wa kujadili uongozi wa Palestina kuanzia Ukingo wa Magharibi hadi Ukanda wa Gaza," alisema Haniyeh.

**DW**



Mgombea wa urais nchini DRC, Dk. Denis Mukwege, akiwasalimia wafuasi wake wakati alipowasili kwenye mkutano wake wa kampeni eneo la Bukavu. **PICHA: AFP**

## Joto la uchaguzi lazidi kupanda DRC

**KINSHASA, DRC**

WAKATI zimebaki siku saba kabla ya kufanyika kwa zoezi la upigaji kura nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wagombea kiti cha urais wanatoleana vumbi katika majimbo mbalimbali kwa ajili ya kujinadi.

Hata hivyo tatizo la wagombea kutoaminiana na mapigano yanayoendelea mashariki mwa DRC limeongeza hali ya wasiwasi wa zoezi hilo kufanyika kwa njia ya utulivu.

Desemba 20, wapiga kura milioni 44 wataingia katika vyumba vya kura, kati ya milioni mia moja vya taifa hilo.

Changamoto kubwa itakuwa kukosekana kwa miundombinu, kwani nchi hiyo ina kilomita milioni 2.3 ya eneo ambayo haina barabara.

Kulingana na Tume ya Uchaguzi ya DRC (CENI), zaidi ya wagombea 100,000 wanawania nafasi mbalimbali ikiwamo ubunge na udiwani na 22 kwa nafasi ya urais.

Hata hivyo Tume ya Uchaguzi inaendelea kuhakikisha vifaa vya kupigia kura vinasambazwa haraka ikiwamo mashine za kielektroniki, kadi za kupigia kura na vifaa vingine vilivyotengenezwa barani Asia. Shehena ya mwisho iliwasili nchini humo mapema wiki hii.

Hivi karibuni iliripotiwa CENI iliandikia serikali barua ya kutahadharisha kuchelewa kwa ndege nne za Antonov na helikopta kumi za kusafirisha vifaa vya kupigia kura.

**Kulingana na Tume ya Uchaguzi ya DRC (CENI), zaidi ya wagombea 100,000 wanawania nafasi mbalimbali ikiwamo ubunge na udiwani na 22 kwa nafasi ya urais.**

# Mkuu wa polisi Haiti atembelea Kenya

**NAIROBI, Kenya**

MKUU wa jeshi la polisi wa Haiti, Frantz Elbe amefanya ziara nchini Kenya katika kukamilisha mpango wa kupeleka kikosi cha kulinda usalama cha kimataifa nchini mwake katika kusaidia kupambana na magenge ya kihalifu.

Ujumbe wake Elbe utakuwa nchini humo kwa siku tatu na utakutana na mkuu wa jeshi la polisi wa Kenya, Japhet Koome na maofisa wengine wakuu wa usalama.

Ziara hiyo ni sehemu ya maandalizi ya kupeleka zaidi ya askari 1,000 kutoka Kenya kama ujumbe wa Kimataifa wa Kusaidia Usalama (MSS), wa Umoja wa Mataifa uliidhinisha miezi miwili iliyopita.

Kulingana na gazeti la The Star, kikosi cha kwanza cha askari 300 kimepangwa kuwasili Haiti, mnamo Februari mwakani.

Mwezi uliopita, bunge la Kenya liliidhinisha kupelekwa kwa wanajeshi hao, lakini mahakama kuu ilizuia utekelezwaji wake baada ya kuwepo kwa pingamizi la mpango huo.

Mpango huo umekosolewa vikali kutokana na Kenya kuwa na rekodi mbaya ya ukiukwaji wa haki unaofanywa na jeshi la polisi.

Kiongozi wa upinzani nchini humo, Raila Odinga, amelaani mpango huo akieleza hauna tija kwa taifa, lakini Rais William Ruto alitetea akisema Afrika ina nia ya kuchangia uhuru na usalama wa Haiti.

Nchini Haiti kuna magenge 300 yanayoendesha harakati zake katika maeneo mbalimbali na mji mkuu wa Port-au-Prince, wameudhibiti kwa zaidi ya asilimia 80.

**BBC**

# TFF YAKOSHWA USHINDANI NGAO YA JAMII WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limefurahishwa na kufana kwa mechi za michuano ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake zilizochezwa mwishoni mwa wiki iliyopita kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na kushuhudiwa Simba ikitawazwa mabingwa.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana shirikisho hilo pia limekoshwa na ushindani ulioonekana katika mechi zote nne, viwango bora, pamoja na hamasa ya hali ya juu kwa mashabiki kwenye kuzishangilia timu zao.

Ndimbo aliwashukuru wachezaji, wadau, klabu na mashabiki wote waliojitokeza na kuifanya michuano hiyo kama sherehe au mtoko wa familia, na kuongeza baada ya kumalizika, sasa rasmi Ligi Kuu ya Soka Wanawake msimu wa 2023/24 imefunguliwa.

"Kiujumla mechi zote za Ngao ya Jamii zilikuwa nzuri na bora, tumeona mechi mbili za nusu fainali, mechi ya kutafuta mshindi wa tatu na fainali, tukiangalia ubora wa mechi, ushindani, wachezaji mmoja mmoja na hamasa kutoka kwa mashabiki ni kubwa sana.

Mechi zilikuwa ngumu, wachezaji walivyokuwa wakishindana, angalia mechi ya fainali kati ya Simba Queens na JKT Queens, tulipaata fainali bora kabisa, ilikuwa na ushindani wa hali ya juu," alisema Ndimbo.

Ofisa huyo wa TFF aliwasifu mashabiki waliokuwa wakijitokeza uwanjani kuzishangilia timu zao akisema ni kitu kingine kilichosababisha michuano hiyo iwe ya kuvutia na ya kipekee.

Aliongeza wazo la michuano hiyo ya Ngao ya Jamii kuchezwa na mfumo huo mpya nalo lilikuwa bora.

"Ni shindano lililochezwa kwa mara ya kwanza katika historia ya soka la wanawake Tanzania na inaonyesha kulikuwa na wazo bora la kufanya hivyo kwenye mfumo huu mpya, limekuja katika wakati bora, tunawashukuru mashabiki na wadau mbalimbali waliojitokeza na timu zote kwa kutupatia kiwango bora, sasa tunasema rasmi Ligi Kuu ya Wanawake imeanza," Ndimbo alisema.

Simba Queens ilibeba taji hilo kwa kuifunga JKT Queens penalti 5-4 baada ya kumaliza dakika 90 kwa sare ya bao 1-1, nafasi ya tatu ilienda kwa Yanga Princess ambao waliwafunga Fountain Gate Princess penalti 4-2 baada ya kutoka suluhu.




Mshindi wa Kampeni ya KrismasiNaSportPesa, John Ntigonza (kulia), akikabidhiwa zawadi yake ya Sh. 100,000 na Mwakilishi wa Kampuni ya SportPesa, Lydia Solomon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafunzo yatamba kuichapa Mlandege

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KIKOSI cha Maafande wa Mafunzo SC kinatarajia kukutana na Wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi katika mechi ya mzunguko wa 15 wa Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Mau A.

Mafunzo itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuchapwa katika mechi mbili zilizopita lakini pia ikiwa na matokeo ya kusuasua msimu huu.

Kocha Mkuu wa Mafunzo, Abdallah Bakari, alisema kwa sasa kikosi chake kimeimarika na anaamini ataanza kupata matokeo chanya katika mechi za ligi hiyo kuanzia leo.

Bakari alisema bado malengo ya timu yake ni kumaliza ikiwa katika nafasi za juu katika msimamo wa ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ).

Kocha huyo alisema hana hofu yoyote kuelekea mechi hiyo na baada ya ligi kusimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yataambatana na kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili na uhamisho wa wachezaji.

"Kipindi chote ambacho ligi itasimama itatusaidia kwa kiasi kikubwa kufanya maandalizi ya kujiimarisha na mzunguko wa lala salama. Ni kawaida katika Ligi yenye ushindani kuwa na mwanzo mbaya lakini pia ukawa na mwisho mzuri.

Sisi tumeanza vibaya sana msimu huu na wachezaji hawakukata tamaa, lakini tunashukuru mwisho mwa mzunguko tumepata matokeo ambayo yamesaidia kututoa katika mstari mwekundu," alisema kocha huyo.

## Tukuyu Sound yaja na tatu za 2023/24

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya Tukuyu Sound ya jijini, Dar es Salaam imekamilisha nyimbo tatu mpya maalumu kwa ajili ya kufungia mwaka 2023, imeelezwa.

Nyimbo hizo mpya ni pamoja na Fumbo, Ngwangwa Na Chini ya Jua.

Mkurugenzi wa bendi hiyo, Kalala Junior, alisema jana tayari nyimbo hizo zimeanza kusikika mapema mwezi huu katika maonyesho mbalimbali ya bendi hiyo yanayoendelea.

"Tuna nyimbo hizo tatu za kufungia mwaka 2023 na kuukaribisha 2024, nyimbo hizo zimepangiliwa kwa ufundi wa hali ya juu na zimekubalika mapema kwa mashabiki wetu hata kabla hatujaingia studio kuzirekodi," alisema Kalala Junior.

Aliongeza kwa kawaida nyimbo mpya zinapopigwa katika kumbi za burudani na kukubalika haraka, ni dalili njema kwao zitafanya vizuri sokoni.

## Dodoma Jiji yawaza pointi sita Ligi Bara

**Na Saada Akida**

WAKATI dirisha dogo la usajili wa wachezaji limefunguliwa leo, Kaimu Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Kassim Lyogope, amesema akili na mawazo yake kwa sasa ameelekeza kuhakikisha anavuna pointi sita kutoka katika mechi mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara zinazofuata dhidi ya Ihefu FC na Mashujaa FC.

Lyogope aliliambia gazeti hili anahitaji kupambana ili kushinda mechi hizo zinazofuata halafu ndio ataanza mipango ya kuboresha kikosi chake kwa ajili ya kufanya vyema katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema anaamini akipata ushindi katika mechi hizo mbili atafikisha pointi 21 ambazo zitawatoa kwenye nafasi ya tisa na kupaa hadi nafasi ya tano au nne kwenye msimamo wa ligi hiyo ya juu nchini.

"Tutalazimika kufanya usajili lakini kwa sasa ni mapema kuweka wazi ni maboresho yapi tutayafanya, ila baada ya tathmini yetu tutaweka wazi. Lakini pia tunakibarua kigumu cha mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Magereza ya Dar. Tumejipanga kufanya vizuri katika michuano hiyo," alisema kocha huyo.

Aliongeza licha ya kukutana na timu ya daraja la chini, lakini kikosi chake kimejipanga kukabiliana na ushindani na ugumu wa aina yoyote kwa sababu mechi za mtoano huwa na changamoto mbalimbali.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### VARANE KUONDOKA UNITED

KLABU ya Manchester United iko hatarini kumpoteza Mfaransa Raphael Varane mwenye umri wa miaka 30 kwa uhamisho wa bila malipo msimu ujao huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwaka mmoja mapema kuliko ilivyotangazwa hapo awali. **(Athletic)**

### BARCA YAMTAKA GREENWOOOD

BARCELONA na klabu nyingine kubwa Ulaya zinamfuatilia mshambuliaji wa Manchester United na England, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 22, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo wa msimu mmoja huko Getafe. **(Talksport)**

### OSIMHEN, NAPOLI WATETA

NAPOLI imefanya mazungumzo na mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24 kuhusu kuongeza mkataba mpya utakaomweka klabuni hapo hadi mwaka 2026, ikiwa pamoja na kipengele cha kumwachia cha pauni milioni 115. **(Sky Sports Italia)**

### TEN HAG HAFUKUZWI

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, hayuko hatarini kutimuliwa kwa sababu klabu hiyo haitaki kufanya uamuzi wowote mkubwa hadi mauzo yanayotarajiwa ya hisa asilimia 25 kwa bilionea, Sir Jim Ratcliffe, kutatuliwa. **(Independent)**

### POTTER ATAJWA UNITED

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter, anapigiwa upatu kuchukua nafasi ya Erik Ten Hag katika klabu ya Manchester United. **(Sun)**

### LOPETEQUI AINGIA SOKONI

KOCHA wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui, pia yuko katika nafasi nzuri ya kurithi mikoba ya Erik Ten Hag ikiwa klabu hiyo ya Old Trafford itaamua kuachana na Mholanzi huyo. **(Relevo)**

### KIWIOR ANUKIA MILAN

AC Milan ipo katika mazungumzo na Arsenal kuhusu mkataba wa mkopo kwa beki wa Timu ya Taifa ya Poland, Jakub Kiwior, mwenye umri wa miaka 23. **(Calciomercato)**

### ELVEDI ANUKIA CHELSEA

MLINZI wa Borussia Monchengladbach na Uswisi, Nico Elvedi, mwenye umri wa miaka 27 anaonekana kulengwa na Chelsea ifikapo Januari baada ya jeraha lingine kwa beki wa pembeni wa England, Reece James (24). **(Teamtalk)**

### CASEMIRO, MARTIAL KUUZWA

KUSHINDWA kufuzu hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kumeacha pengo la pauni milioni 28 katika bajeti ya uhamisho ya Manchester United na huenda ikamaanisha iko tayari kupokea maombi ya kumuuza kiungo wa kati wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 31, mshambuliaji wa Ufaransa na Anthony Martial (28). **(Mail)**

### CHELSEA KUMUUZA MAATSEN

CHELSEA ipo tayari kumuuza beki wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 21, wakati wa uhamisho wa dirisha la usajili la Januari. **(Mirror)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TORRES: BARCELONA IKO HATARINI KUANGAMIZWA

●●●Lakini nyota huyo asema bado wako hai, watabadilisha upepo...

**BRUSSELS, Ubelgiji**

FERRAN Torres amesema watu wanataka "kuiangamiza" Barcelona baada ya mabingwa hao wa Hispania kupokea kichapo cha nne katika michezo tisa huku pia ikipoteza 3-2 dhidi ya Antwerp kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hapo juzi usiku.

Barca walikuwa tayari wametinga hatua ya 16 kama washindi wa kundi baada ya Shakhtar Donetsk kufungwa na FC Porto katika mchezo mwingine wa Kundi H, lakini kupoteza huko kuliongeza shinikizo kwa Kocha, Xavi Hernandez baada ya kufungwa mabao 4-2 na Girona kwenye LaLiga Jumapili iliyopita.

Torres alitoa maoni yake kwa Barca, ambao wamepitwa pointi saba kutoka kileleni katika msimamo wa LaLiga, lakini bado wako hai katika mashindano manne, kuwa watabadilisha mambo.

"Tuko pamoja na kocha na mawazo yake hadi mwisho," alisema Torres akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ni rahisi kumkosoa kocha, lakini wachezaji ndio wapo uwanjani. Tunajua jinsi mambo yanavyokwenda Barca, watu wa nje wanajaribu kutuangamiza, kutufanya tuwe na wasiwasi, lakini tutageuza mambo. Kuna siku zote. kelele nyingi za nje, lakini lazima tuishi na hilo."

Arthur Vermeeren aliipatia Antwerp bao la kuongoza dakika ya pili kwenye Uwanja wa Bosuilstadion kabla ya Torres kuisawazishia Barca kabla ya mapumziko.

Vincent Janssen alirejesha uongozi kwa Antwerp, lakini Marc Guiu mwenye umri wa miaka 17 alisawazisha kwa timu hiyo ya Katalunya.

Hata hivyo, kulikuwa na mabadiliko ya mwisho pale fowadi wa Nigeria, George Ilenikhena, pia mwenye umri wa miaka 17, alipofunga bao katika dakika ya 92 na kuifanya Antwerp kupata pointi tatu za kwanza katika mashindano ya msimu huu.

"Ndio, nina wasiwasi, tuko kwenye mwendo mbaya, hayo ni matokeo mabaya mawili mfululizo," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Lazima tujikosoe, tujipange zaidi, timu zinatengeneza nafasi dhidi yetu na tunapambana kutengeneza za kwetu.

"Wachezaji hawakuwa katika kiwango chao bora leo (juzi), lakini sipendi kuzungumza vibaya kuhusu watu binafsi. Wana zaidi ya wanavyoonyesha. Makosa ya mtu binafsi yanatugharimu."

# SANCHO KUBADILISHWA NA RAPHINHA WA BARCA




**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United inafikiria kumtoa winga wao, Jadon Sancho kama sehemu ya mabadilishano na Raphina wa Barcelona wakati wa dirisha lijalo la majira ya joto.

Sancho mwenye umri wa miaka 23 amekuwa akihusishwa na timu mbalimbali tangu kuibuka taarifa za kuondoka baada ya kupishana kauli na kocha wake, Erik Ten Hag.

Tangu dirisha lililopita Raphinha (26), amekuwa akitajwa ataondoka Barcelona, lakini ni kwa kuuzwa ili kupata fedha itakayotumika kufanya usajili wa timu.

Hata hivyo, Raphinha mwenyewe mara kadhaa amekuwa akipinga suala hilo na kusisitiza bado anahitaji kuendelea kusalia Barca.

Kwa sasa Raphinha ni mmoja kati ya nyota tegemeo katika kikosi cha kwanza cha wababe hao kutoka Nou Camp na tangu kuanza kwa msimu amecheza mechi 15 za michuano yote na kutoa asisti tano.

Wakati Sancho ambaye kwa sasa anatanya mazoezi na kikosi cha akiba, msimu huu amecheza mechi tatu za Ligi Kuu England.

# Haaland kutafutiwa mbadala

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City itaingia sokoni katika dirisha la Januari 2024 ili kusajili mshambuliaji mpya endapo Erling Haaland ataendelea kusumbuliwa na majeraha.

Haaland aliukosa mchezo wa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Luton Town kwenye Ligi Kuu England mwishoni mwa wiki na Kocha, Pep Guardiola alisema mshambuliaji wake huyo anasumbuliwa na maumivu ya mguu.

Guardiola alisema mshambuliaji huyo atahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina na kutazama maendeleo yake siku kwa siku au wiki kwa wiki ili kujua ukubwa wa tatizo.

Haaland pia alikosa mechi ya mwisho ya hatua ya makundi la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati City ilipoifunga mabao




3-2 FK Crvena Zvezda huko Serbia.

Lakini Guardiola anaamini Haaland atakuwa tayari kwa ajili ya michuano ya Klabu bingwa ya Dunia itakayofanyika huko Saudi Arabia, Desemba 19.

"Siku iliyofuata baada ya ile mechi ya Aston Villa, Haaland hakuwa anatembea vizuri" alisema Guardiola.

"Nilizungumza naye alisema anaendelea vizuri, lakini daktari alisema anahitaji kufanyiwa uchunguzi kwa ukaribu zaidi."

Hata hivyo, City itaingia sokoni kusaka mshambuliaji mpya kwenye dirisha la Januari 2024, kwa kile kinachoelezwa kama Haaland ataonekana ana shida kubwa.

Haaland amekuwa muhimu kwenye kikosi cha City akifunga mabao 71 katika mechi 75 alizocheza za michuano yote.

# Pochettino ataka wapya Chelsea

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Mauricio Pochettino, ameripotiwa ana mpango wa kufanya usajili wa wachezaji wasiopungua watatu kwenye dirisha lijalo la uhamisho wa Januari, 2024.

Wakati The Blues ikiwa bado haijapata kasi yake tangu kocha huyo kutoka Argentina alipotua Stamford Bridge, timu hiyo kwa sasa inashika nafasi ya 12 msimamo wa Ligi Kuu England.

Kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Everton katika mechi iliyochezwa Jumapili iliyopita kiliifanya Chelsea kupoteza mechi tatu kati ya nne za mwisho, huku ikipata vichapo vingine vikitoka kwa Newcastle United na Manchester United.

Baada ya kipigo cha Goodison Park, Pochettino alisema kikosi chake kinahitaji sura mpya za kuongeza nguvu kwenye dirisha la Januari, licha ya Chelsea kutumia zaidi ya pauni bilioni moja kwenye usajili wa madirisha matatu yaliyopita.

Pochettino wala hajali hilo na kutaka mabosi wa timu hiyo kufanya usajili wa mastaa watatu wakati dirisha litakapofunguliwa na ameweka wazi anahitaji beki wa kati, kiungo wa kati na mshambuliaji ili waje kuongeza nguvu na kuboresha ubora wa kikosi chake.

Licha ya Chelsea kufunga mabao 26 katika mechi 16 kwenye Ligi Kuu England msimu huu, bado kiwango chake cha kufunga si bora sana, huku mshambuliaji wao, Nicolas Jackson, bado anajitafuta, hajaonyesha makali yake tangu alipotua kutoka Villarreal.

Mshambuliaji, Armando Broja anarejea kwenye kikosi taratibu akitokea kwenye majeruhi, huku Christopher Nkunku akiwa hajacheza mechi yoyote kutokana na kusumbuliwa na maumivu ya goti, hivyo Chelsea inakosa nguvu kwenye eneo lake la ushambuliaji.



HABARI MICHEZO

# TIGO YAKABIDHI MAMILIONI MSHINDI MAGIFT DABODABO

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mbezi, Rehema Makunganya ambaye ni Mama Lishe katika Soko la Mapinduzi Mwananyamala, Dar es Salaam amekabidhiwa zawadi ya Sh. milioni 10 na Kampuni ya Tigo baada ya kuibuka mshindi katika kampeni ya Magift dabodabo, inayoendelea.

Akizungumza baada ya kukabidhi hundi ya mfano, Meneja wa Tigo Kanda ya Dar Es Salaam, Beatrice Kinabo, amewasisitiza wafanyabiashara na Watanzania kufanya miamala mbalimbali kwa kutumia TigoPesa ili kuibuka washindi wa kampeni hiyo ambayo bado inaendelea.

"Muda huu tunaozungumza kuna washindi 15 wapo Dubai wanakula "bata", wengine wapo Zanzibar na kuna wengine wamejishindia fedha taslimu, wapo pia wamejishindia vifaa vya Hisense kwa hiyo kampeni bado inaendelea. Nawaomba wateja wetu endeleeni kufanya miamala na Tigopesa kwa wingi, lipa kwa simu, nunua vifurushi ili utengeneze mazingira ya kuibuka mshindi, "alisema Beatrice.

Mshindi wa zawadi hiyo, Rehema, alisema hakuamini alipopewa taarifa ya kushinda fedha hizo.

"Mara ya kwanza napigiwa simu na kuambiwa nimeshinda Sh. milioni 10 ya magift dabodabo sikuamini kwa kweli, nilijua ni utapeli lakini baadaye nikaja kuamini baada ya kuona kumbe nimepigiwa na namba 100, nawasihi Watanzania tumieni Tigo, fanyeni miamala maana ndio siri ya ushindi, nilikua na genge lakini sasa naenda kufungua mgahawa mkubwa" alisema Rehema.

Aliongeza anawaomba watu wengine kutokata tamaa kwa sababu kampeni hiyo ni ya kweli na zawadi kwa washindi zinatolewa mapema.




Meneja wa Kampuni ya Tigo Kanda ya Dar es Salaam, Beatrice Kinabo (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 mshindi wa Kampeni ya magifti dabo dabo, Rehema Makunganya jijini jana. **PICHA : MPIGAPICHA WETU**

# Boy Cylla atwaa taji la Rising Star Online

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msanii wa Hip Hop, Sailas Mwakabana (Boy Cylla) wa Dar es Salaam ameibuka mshindi wa kwanza katika mashindano ya kusaka vipaji vya muziki ya Rising Star Online Competition, serikali imeonya wasanii ambao wanakiuka maadili ya Kitanzania.

Mwakabana ameibuka mshindi baada ya kuwashinda wasanii wawili waliongia hatua ya fainali, Christian Job wa Iringa na Yusuph Hussein wa Dar es Salaam.

Kwa ushindi huo, Boy Cylla alizawadiwa zawadi yya Sh. milioni moja na kupata nafasi ya kurekodi video, audio za nyimbo zake pamoja na kulipiwa gharama nyingine zenye thamani ya Sh. milioni tisa katika studio ya Bongo Records.

"Nimefurahi sana kushinda nafasi ya kwanza, ushindani ulikuwa mkubwa sana, nawapongeza washiriki wenzangu wote kwa kuleta changamoto ambayo ilinifanya niongeze bidii na kuibuka mshindi," alisema Boy Cylla.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, amewaonya wasanii wanaokiuka maadili ya Kitanzania na kurudisha nyuma sekta ya muziki nchini.

Msigwa alisema sekta ya muziki kwa sasa inakuwa kwa kasi na takwimu zinaonyesha zinachangia katika ukuaji wa uchumi kwa asilimia 19, lakini bado baadhi ya wasanii wanakiuka maadili na kuwakimbiza wawekezaji.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Radian, Freddie Manento, alisema wamefurahi kutoa fursa kwa vijana kushiriki na kuonyesha vipaji vyao na kuongeza shindano hilo litafanyika kila mwaka.

"Nawapongeza wadhamini mbalimbali kama benki ya CRDB, Letshego Faidika, FASTHUB, PrintPro, Tanzanie General, MMDT na hoteli ya Giraffe kwa kufanikisha shindano hili," alisema Manento.

## Mbangossoum katika hesabu za Benchikha

INATOKA UK. 24

"Tunahitaji ushindi na tutacheza kwa kuwaheshimu wapinzani wetu, kwa upande wangu hii mechi ni muhimu sana baada ya hapa nitaifikiria Wydad Casablanca. Hakuna mechi rahisi na kila mchezo umekuwa na maandalizi yake.

Kuwapo kwa mfululizo wa mechi kila baada ya siku mbili au tatu hilo halitakuwa na athari, kikubwa ni kuandaa timu kulingana na mpinzani unayekwenda kucheza naye," alisema Benchikha.

Kipa wa timu hiyo, Ally Salim, alisema wamejiandaa vizuri kwenda kuwakabili wapinzani wao na watapambana kuhakikisha wanafanikiwa kuvuna pointi tatu muhimu.

"Tumejipanga vizuri, wachezaji wote tunajuana, hautakuwa mchezo rahisi kwa kila upande, lakini tunaahidi furaha kwa mashabiki wetu," Salim alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema wamefanya maandalizi mazuri na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kuwavaa Wekundu wa Msimbazi.

Alisema utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu ya wapinzani wao bado wako katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo wataingia kuwavaa kwa heshima kubwa.

"Hatutaingia kwa kuibeza kwa sababu Simba wanacheza mechi mfululizo, wako fiti sana na wameimarika, hatutakiwi kamwe kuingia uwanjani kwa kuwabeza, tofauti na sisi tunakaa muda mrefu. Simba imekutana na timu kama Al Ahly ambayo wanatoka nao sare kwa hiyo sio timu ya kuingia kirahisi rahisi kwa sababu ya ubora wao," alisema Maxime.

Aliongeza ujio wa Benchikha katika kikosi cha Simba hautawatia hofu kwa sababu wachezaji ndio wenye jukumu la uwanjani na kocha kazi yake ni kufundisha.

Nahodha wa Kagera Sugar, Khamis Kiiza alisema mechi hiyo itakuwa na ushindani na wao wamejipanga kutafuta matokeo mazuri.

## Wachezaji Yanga waitisha Mtibwa

INATOKA UK. 24


kufanya vizuri kuwapa raha," alisema Mauya.

Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, alisema maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na sasa wanasubiri muda wa kuanza mchezo huo ambao wamejiandaa kuonyesha ubora wao.

"Kikosi kimeshajiandaa na mechi husika, kinaweza kuwa na maoni tofauti kulingana na mpinzani tunayekutana naye, lakini kwetu tunamheshimu kila tunayekutana naye, hata kama Mtibwa Sugar yupo mkiani sisi tunaichukulia ni moja kati ya timu bora, tutakwenda kucheza kwa ubora wetu kuhakikisha tunapata pointi tatu," alisema meneja huyo.

Torres: Barcelona iko hatarini kuangamizwa UKURASA 21

Michezo
Ijumaa Desemba 15, 2023
Nipashe





# MBANGOSSOUM KATIKA HESABU ZA BENCHIKHA

Yupo pia Chasambi, Lawi wakati Simba ikiikaribisha Kagera Sugar leo...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba inatarajia kuwakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, klabu hiyo inatajwa kukamilisha mazungumzo ya kuwasajili wachezaji wapya watatu akiwamo nyota, Eric Mbangossoum kutoka Union Sportif ya Morocco.

Wachezaji wengine wanaohusishwa kutua Msimbazi katika dirisha dogo la usajili ambalo limefunguliwa rasmi leo ni Lameck Lawi kutoka Coastal Union na Ladack Chasambi wa Mtibwa Sugar, zote za hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ni mapema kusema lolote kwa sasa na ameweka wazi mchakato huo wa usajili unasimamiwa na Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, ambaye ndiye amefanya tathimini ya kubaini eneo gani anahitaji kuongeza nguvu.

Ahmed alisema mchakato huo utafanyika kwa utulivu na wanaamini Benchikha atasajili wachezaji ambao watasaidia timu kufikia malengo ya klabu.

"Kwa sasa ni mapema sana kuzungumza lolote juu ya usajili, kujua nani anaingia au anatoka, hilo ni jukumu la kocha ambaye amefanya tathmini ya timu yake na tunatarajia kupata mapendekezo ya nafasi na idadi ya wachezaji watatua kuongeza nguvu.

Muda ukifika kila kitu kitawekwa wazi, kwa sasa akili na nguvu zinaelekea katika mechi zilizopo mbele yetu, tunakibarua kigumu cha kutafuta pointi tatu dhidi ya Kagera Sugar na baada ya hapo kuna kuwapeleka moto Wydad Casablanca hapa nyumbani na kuacha alama ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema Ahmed.

Kuelekea mechi dhidi ya Kagera Sugar, Benchikha alisema baada ya safari ndefu kutoka Morocco wamerejea na kufanya maandalizi mazuri kwa ajili ya kuvuna alama tatu katika mchezo huo muhimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Benchikha alisema amepata fursa ya kuona taarifa za wapinzani wao na ameandaa vizuri kikosi chake kwa ajili ya kucheza soka la ushindani kutokana na ubora wa wapinzani wao.

INAENDELEA UK. 23

# Wachezaji Yanga waitisha Mtibwa


Musonda (kushoto) na Skudu

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga ambao bado wana 'joto' la michuano ya kimataifa, Dickson Job na Zawadi Mauya, wametamba timu yao iko kamili kuhakikisha inapata ushindi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Wakizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzao, Job, alisema wanaamini watapata ushindi katika mechi hiyo na siri itakayowapa matokeo chanya ni ubora wa kikosi chao.

"Hatusemi hivi kwa sababu Mtibwa Sugar imekuwa haifanyi vizuri katika mechi ya Ligi Kuu, la hasha, ila tuna jukumu la kuhakikisha tunawapa furaha wanachama na mashabiki wa klabu yetu, pamoja na kurejea kileleni tulipopazoea," alisema Job.

Aliongeza mechi hiyo itakuwa ni kipimo kizuri kuelekea katika mechi ya raundi ya nne ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama kutoka Ghana itakayochezwa Desemba 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es salaam.

"Tunaamini utakuwa mchezo mgumu, Mtibwa hajapata matokeo mazuri mechi za nyuma, kwahiyo tunajua watakuja kupambana ili kuondoa hali hiyo, wachezaji wa Yanga tunalijua hilo kwa hiyo na sisi tutapambana ili kushinda turejee juu ya msimamo wa ligi, naamini tutawapa furaha wanachama na mashabiki wa Yanga," aliongeza beki huyo.

Mauya alisema licha ya Mtibwa kutofanya vizuri, bado wanaamini ni moja ya timu kubwa hapa nchini, hivyo hawataingia uwanjani kwa kubweteka.

"Mtibwa ni timu kubwa, siyo timu ndogo na kwa sababu sisi tunatarajia kucheza mechi ya kimataifa, nadhani hiki kitakuwa ni kipimo cha kutosha kabisa, tunaomba tu mashabiki wajitokeze kwa wingi, waje kutupa sapoti, unajua wanapotushangilia ndipo na sisi tunacharuka uwanjani na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >